# Nipashe

MWANGA WA JAMII

Ijumaa Septemba 11, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580335

The Guardian digital


www.ippmedia.com

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710




## Ilani ya CUF yaibua tena fao la kujitoa, baraza dogo la mawaziri

UKURASA 2


Tukienzi Kiswahili basi kama tumeamua

BUFE

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA

Uwekezaji UTT unavyookoa kipindi cha ukata

UCHUMI

Wasomi UDSM kuanza kupikwa kiujasiriamali

•Ni ili kuwaondolea kiu ya kuajiriwa

•2021 wahitimu 250 kuonyesha matunda

UKURASA 11

# Mgombea wa ubunge CHADEMA matatani



Mgombea ubunge Jimbo la Singida Mjini kupitia CHADEMA, Rehema Mkoha (kushoto), akizungumza na waandishi wa habari mjini Singida jana, kuhusu tukio la kupekuliwa na polisi nyumbani kwake juzi. Kulia ni Aneth Juma akiwa amefunga bandeji mguuni kwa madai ya kupigwa na polisi, wakati wa kumsaka Mkoha. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

**ADAIWA** kumiliki silaha isivyo halali, polisi wapekua nyumba yake...

*Endelea ukurasa 2*

## Wafungwa miaka miwili kumwomba rushwa 500,000/- mganga wa jadi

UKURASA 3

## EWURA YAZIFUTIA LESENI KAMPUNI 4 ZA MAFUTA

UKURASA 3

MICHEZO VILLA YAJIANDAA KUMUUZA SAMATTA UK.24

MAONI, KATUNI UK.6


**Fursa kwa Wagombea! 2020**

VOTE

Gazeti la Nipashe linawapongeza wateule wote waliopitishwa na vyama vyao kugombea ubunge katika majimbo mbalimbali nchini

Je ungependa kukishukuru chama chako ?

Je ungependa kutangaza sera zako kwa wapiga kura ?

Nipashe inatoa nafasi kutangaza sera zako kwa gharama nafuu

Nipashe MWANGA WA JAMII

Wasiliana nasi

Simu: 0686 101335,

Barua pepe: advertise@guardian.co.tz

VOTE

# Mgombea ubunge CHADEMA mbaroni madai kumiliki silaha

**Na Mwandishi Wetu**

JESHI la Polisi mkoani Singida limemkamata mgombea ubunge Jimbo la Singida Mjini kupitia Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Rehema Mkoha, na watu wengine 10 kwa madai ya kumiliki silaha kinyume cha sheria.

Mkoha alikamatwa baada ya Jeshi la Polisi kupata taarifa kuwa nyumba anayoishi anamiliki silaha za moto bila kuwa na vibali.

Tukio hilo limetokea siku chache tangu chama hicho kizindue kampeni zake za uchaguzi ngazi ya mkoa zilizofanyika kiwanja cha Bombadia na kuhudhuriwa na mamia ya wananchi na wafuasi wa chama hicho.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Singida, Sweetbert Njewike, akizungumza na gazeti hili kwa simu jana, alikiri kukamatwa kwa mgombea huyo na watu wengine na kisha kuachiwa kwa dhamana baada ya kuhojiwa na kwamba watatakiwa kuripoti tena polisi leo.

Njewike alisema kabla ya kuwakamata, walifanya upekuzi ndani ya nyumba ya mgombea huyo baada ya polisi kupata taarifa kuwa anamiliki silaha ya moto. Hata hivyo majina ya watu wengine waliowakamata hakuyataja.

"Tulipomkamata mgombea huyo na vijana wengine wanaoishi ndani ya nyumba hiyo, tuliwaachia kwa dhamana na tunaendelea na uchunguzi. Tumewaambia waje kesho (leo) kwa mahojiano zaidi," alisema Kamanda Njewike.

Mgombea ubunge huyo, awali aliileza gazeti hili kuwa usiku wa kuamkia juzi saa 8.30 usiku, baada ya kumaliza kikao chao cha kujipanga kwa ajili ya kuendelea na mikutano ya kampeni, alishtuka kusikia milango ikigongwa kwa nguvu huku wakiamuriwa wafungue.

Alisema alitoka chumbani kwake na vijana wake na kuwaona watu huku mmoja akiwa ameshika mtutu wa bunduki, hivyo wakawa wanajiuliza wafanyaje kwa kuwa kwa jinsi walivyo ni lazima wataingia ndani na hawakuwa na uwezo wa kupambana nao.

"Wakati narudi chumbani kwangu watu hao walifanikiwa kubomoa mlango wa mbele na kuingia ndani na moja kwa moja walipitiliza kwenye vyumba mbalimbali na walipofika kwenye chumba changu walikuta nimefunga mlango ili niweze kutoa taarifa kwa watu wengine na wakati napiga simu ndipo walipouvunja mlango wa chumba changu," alidai Mkoha.

Alisema wakati huo alikuwa amejificha bafuni ambapo walimkamata mtu mmoja aliyekuwa naye chumbani, aliyemtaja kwa jina la Aneth na kuanza kumpiga sehemu mbalimbali za mwili wake na kumjeruhi.

Mkoha alisema baada ya hapo, walimkamata huku mmoja wao akimwelekeza mtutu wa bunduki na mwingine akimshambulia mara nne kwa kutumia gongo na baadaye walitolewa na kuwekwa sebuleni ambako walianza kuwahoji na kujitambulisha kuwa ni askari polisi na kwa nini walipokuwa wakigonga mlango hawakuwafungulia.

Katika kundi la watu hao, alisema alikuwapo Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Unyakumi aliyemtaja kwa jina la Mossy Athuman. Alisema watu hao walichukua maelezo yao na walipomwuliza yeye ni nani, alisema ni mgombea wa ubunge kupitia CHADEMA.

Alisema askari hao waliwaambia kuwa wamefika hapo kufanya upekuzi baada ya wasiri wao kuwaeleza wanamiliki silaha za aina mbalimbali.



Mgombea mwenza wa kiti cha urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa tiketi ya CCM, Makamu wa Rais Samia Suluhu Hassan, akimkabidhi kitabu cha Ilani ya Uchaguzi ya 2020/25 mgombea kiti cha ubunge wa Jimbo la Mtwara Vijijini kwa tiketi ya chama hicho, Hawa Ghasia, wakati wa mkutano wa kampeni za uchaguzi mkuu, uliofanyika katika Uwanja wa Polisi Nanyamba, mkoani Mtwara jana. **PICHA: OMR**

# Ilani ya CUF yaibua fao la kujitoa

**Na Elizabeth Zaya**

CHAMA cha Wananchi (CUF) kimesema kuwa iwapo kitapata ridhaa ya kuongoza Tanzania kitahakikisha kunakuwa na fao la kujitoa katika mifuko ya hifadhi ya jamii na mfanyakazi anapata malipo yake ndani ya miezi mitatu.

Aidha, kimesema kitaunda serikali ndogo ya wizara 15 kwa lengo la kupunguza matumizi ili kuelekeza nguvu katika miradi ya maendeleo na kwamba kitapunguza matumizi yasiyo ya lazima na kuanzisha utaratibu wa matumizi ya 'zero budgeting', kuondoa marupurupu na mafao ya viongozi.

Hayo yamo ndani ya Ilani ya chama hicho yenye kurasa 167 inayoelezea vipaumbele ambavyo vitatoa ahueni ya maisha kwa mwananchi wa kawaida.

Kwa mujibu wa ilani hiyo, itatengenezwa mifumo ambayo mifuko ya hifadhi ya jamii ya Shirika la Hifadhi ya Jamii (NSSF) na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF), inawajibika zaidi kwa wanachama.

Ilani hiyo imesema wanachama wanaopoteza ajira na wanaoacha ajira malipo yao (fao la kujitoa) yatakamilishwa katika kipindi cha miezi mitatu na mwanachama atakuwa na haki ya kuchagua utaratibu wa malipo anaoutaka.

Pia imesema sheria itarekebishwa ili mwanachama awe na haki ya kuchukua fedha zake zote kwa mkupuo mmoja iwapo huo ndio utakuwa uamuzi wake.

"Ili kuiboresha mifuko ya hifadhi ya jamii zaidi serikali ya CUF italipa madeni inayodaiwa na mifuko ya hifadhi ya jamii bila kuchelewa, ili kuiimarisha na kuifanya kuwa na utaratibu unaonufaisha wanachama wake," ilieleza ilani hiyo.

Aidha, ilani hiyo imebainisha kuwa mifuko hiyo itawajibika kugawa robo tatu ya faida yote inayotokana na vitega uchumi vilivyotokana na kuwekeza fedha za wanachama, kwa wanachama wa mifuko hiyo.

"Katika mfumo wa demokrasia ya vyama vingi vya siasa, uwezekano wa kuwa na viongozi wakuu wengi wastaafu ni mkubwa sana, na hivyo kulisababishia taifa kuwa na mzigo mkubwa katika kuwahudumia," inaeleza ilani ya chama hicho.

"Mathalani, kwa sasa serikali za CCM (Muungano na Zanzibar) zinahudumia viongozi wakuu wastaafu wasiopungua 30 kwa gharama ya mabilioni ya fedha kila mwaka," inaeleza ilani hiyo.

"Ili kupunguza mzigo kwa wananchi itahakikisha inatumia vizuri fedha za wananchi kwa kupunguza matumizi na gharama zisizo za lazima ili fedha zitakazookolewa zielekezwe zaidi katika kujenga miundombinu ya barabara, reli, umeme, maji, bandari na Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA)."

# CCM yaahidi furaha kwa wajasiriamali

**Na Gwamaka Alipipi,** GEITA

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) kupitia Ilani yake ya Uchaguzi ya mwaka 2020-2025, kimewaahidi kuwanyanyua zaidi vijana, wanawake na makundi ya wajasiriamali kwa kuwapatia mafunzo, stadi za ujasiriamali, usimamizi wa shughuli za kiuchumi na kuwawezesha kurasimisha shughuli zao.

Katika ukurasa wa 24 wa ilani hiyo ambayo inanadiwa na mgombea wa urais kupitia chama hicho, Dk. John Magufuli, kunabainisha kuwa serikali chini ya chama hicho itaanzisha utaratibu wa kuwakopesha vifaa na mitaji wanafunzi wanaohitimu mafunzo ya ufundi nchini kwa masharti nafuu.

Vilevile, chama hicho kimewahakikishia wananchi kuwekewa mazingira mazuri ili kushiriki kikamilifu katika shughuli za maendeleo kwa kipindi cha miaka mitano ijayo.

Mbali na hayo, chama hicho pia kimeweka mkakati wa kuimarisha viwanda nchini, kuhamasisha uanzishwaji wa viwanda vipya vya kuchakata mazao ya kilimo, mifugo, samaki na rasilimali nyingine za maji kwa kutumia taasisi za umma, sekta binafsi na vikundi vilivyosajiliwa na vyama vya ushirika.

Pia, katika kipindi cha miaka mitano ijayo, chama hicho kimepanga kuanzisha vituo vya uendelezaji wajasiriamali kwa lengo la kuwajengea uwezo na kuwawezesha wananchi kupata ithibati za kimataifa ili kupanua wigo wa fursa za ajira na biashara.

Kwenye Ilani hiyo, CCM pia imepanga kuchochea kasi ya ukuaji wa uchumi shirikishi kwa kutoa fursa kwa wananchi wote pamoja na kuinua hali ya maisha.

Katika kipindi cha miaka mitano ijayo chama hicho kimepanga kuanzisha kanzidata ya watoa huduma katika miradi mikubwa ya kimkakati na kutoa elimu kwa umma juu ya ushiriki wa wajasiriamali katika miradi hiyo.

"Kanzidata hii itawezesha kuunganisha sekta binafsi na wawekezaji au wakandarasi na hivyo kuwawezesha kupata masoko ya bidhaa zao na kufanya kazi kwa ubia na kampuni za nje ili kukuza ujuzi na kuhaulisha teknolojia," inabainishwa katika ilani hiyo.

Kuhusu ujenzi wa viwanda, CCM imepanga kujenga ukanda na kongani za viwanda kila mkoa, kulingana mazao na maliasili zinazopatikana katika kila mkoa na fursa za kijiografia kwa mkoa husika.

Vilevile, kinatarajia kuimarisha mazingira ya ujenzi wa viwanda vya kimkakati kwa kufanya mapitio na maboresho ya sera na mikakati mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuendelea kutekeleza mpango kazi wa kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji nchini.

Katika ilani hiyo, viwanda hivyo vimetajwa kuwa ni pamoja na vile vinavyotumia teknolojia itakayotoa ajira kwa watu wengi, lengo likiwa ni kuongeza ajira zitokanazo na uzalishaji wa bidhaa viwandani kutoka 306,180 mwaka huu hadi 500,000 mwaka 2025.

Chama hicho pia kimepanga serikali yake kuendeleza na kujenga viwanda mama vikiwamo vya chuma, dawa na kemikali, ambavyo vitaleta faida nyingi kwa taifa kama vile ajira na uongezaji thamani malighafi za ndani.

# Wafungwa miaka miwili kumwomba rushwa 500,000/- mganga wa jadi

**Na Mary Geofrey**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Babati, imewahukumu Luhanga Mabeshi na Hamisi Gombona kutumikia kifungo cha miaka miwili jela baada ya kuwakuta na hatia ya kuomba na kupokea rushwa.

Watu hao wametiwa hatiani baada ya kuomba rushwa ya Sh. 500,000 na kupokea Sh. 200,000 jambo ambalo ni kinyume cha kifungu cha 15 cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Na. 11 ya mwaka 2007.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Manyara, Holle Makungu, hukumu hiyo ilitolewa juzi na Hakimu Mfawidhi wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Babati, Simoni Kebello.

Alisema hukumu hiyo ilitolewa baada ya kusikiliza ushahidi wa pande zote na kuridhika bila kuacha shaka yoyote na upande wa mashtaka uliokuwa ukiongozwa na Wakili wa TAKUKURU, Evelyne Onditi.

Makungu alisema awali washtakiwa walifikishwa katika mahakama hiyo kwa tuhuma za kudai na kupokea rushwa kutoka kwa mganga wa jadi wilayani Babati (jina linahifadhiwa).

Washtakiwa hao wanadaiwa walifika wilayani hapo kujitambulisha kama wapelelezi kutoka Umoja wa Waganga wa Jadi na Tiba Asili Tanzania (UWAWATA) na kwamba kwa cheo hicho walikwenda kumkagua mganga huyo wakimtuhumu wamemkuta akifanya shughuli za uganga kwa kutumia ramli chonganishi kinyume na taratibu za uganga, hivyo wakamtaka mganga atoe rushwa ili asichukuliwe hatua.

Mganga huyo, alisema kwa kuwa hakuwa anafanya ramli chonganishi kama ilivyodaiwa, aliamua kwenda kutoa taarifa TAKUKURU iliyowafanya kukamatwa kwa watuhumiwa hao wakiwa wameshapokea rushwa ya Sh. 200,000.

Alisema wakati hukumu hiyo inatolewa mshtakiwa Mabeshi hakuwapo mahakamani kwa kuruka dhamana, hivyo mshtakiwa Gambona alipelekwa gerezani kuanza kutumikia kifungo.



Baadhi ya wazazi wa watoto wenye vichwa vikubwa na mgongo wazi, wakihudhuria kliniki maalumu ya bure katika Taasisi ya Tiba ya Mifupa Muhimbili (MOI), jijini Dar es Salaam jana, kuelekea maadhimisho ya miaka 23 ya utoaji huduma ya taasisi hiyo. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# EWURA yafutia leseni kampuni 4 za mafuta

**Romana Mallya na Frank Maxmillian**

BODI ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), imefuta leseni za kampuni kubwa nne za uendeshaji biashara ya mafuta ya petroli kwa jumla.

Meneja Mawasiliano na Uhusiano wa mamlaka hiyo, Titus Kaguo, aliiambia Nipashe jana kuwa, kampuni hizo zimefutiwa leseni kwa mujibu wa sheria.

Alisema sheria ya petroli zinataka mfanyabiashara wa jumla anatakiwa afanye biashara bila kukosa katika kipindi chote cha leseni yake.

"Hawa wanakaa muda mrefu bila kufanya kazi yoyote ndiyo maana wamefutiwa leseni, tunataka unapopewa leseni yako uagize mafuta, hawa hawajaagiza, kampuni hizi zimefutwa baada ya kutangazwa kwa siku 21," alisema.

Kwa mujibu wa tangazo la Mkurugenzi Mkuu wa EWURA, endapo kampuni hizo hazijaridhishwa na uamuzi wa bodi hiyo, wanaweza kukata rufani Baraza la Ushindani.

Tangazo hilo lilisema uamuzi wa bodi hiyo ulitokana na kikao chake cha kawaida cha 155 kilichoketi Agosti 27.

"Maamuzi hayo yalifikiwa baada ya bodi kujiridhisha kuwa kampuni hizo zimeshindwa kufanya biashara ya mafuta kwa jumla kwa mujibu wa kifungu cha 143(1)(a) cha Sheria ya Mafuta, Sura ya 392 na kanuni ya 16(3) ya Kanuni za Petroli, toleo la Gazeti la Serikali Namba 380 la mwaka 2018," lilisema.

# Wanafunzi 92,947 waomba mikopo elimu ya juu

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB), ikitangaza kufungwa kwa dirisha la maombi ya mikopo kwa njia ya mtandao, kwa mwaka wa masomo 2020, maombi ya wanafunzi 92,947 yamesajiliwa.

Mkurugenzi Mtendaji wa HESLB, Abdul-Razaq Badru, alisema jana jijini Dar es Salaam katika taarifa yake kuwa, mfumo huo wa maombi hautaruhusu usajili wa maombi mapya, isipokuwa kwa waombaji 7,500 walioko mtandaoni, ambao hawajakamilisha maombi hayo.

Badru alisema HESLB ilifungua dirisha la maombi kwa njia ya mtandao, kwa muda wa siku 40 kuanzia Julai 21, mwaka huu.

Hata hivyo, alisema kutokana na maoni na maombi ya wazazi, walezi na wanafunzi, bodi iliongeza siku 10 hadi jana, ili kutoa fursa kwa waombaji kukamilisha maombi hayo.

"Leo (jana) Alhamisi saa 6:00 usiku, dirisha la upokeaji wa maombi ya mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu, kwa mwaka wa masomo 2020/21 kwa njia ya mtandao, litafungwa rasmi. Baada ya muda huo, usajili mpya kwa ajili ya maombi mapya hautaruhusiwa," alisema Badru katika taarifa hiyo.

Badru pia alisema Oktoba Mosi, mwaka huu, HESLB itaanza uchambuzi wa maombi hayo na baadaye itaorodhesha maombi yote yenye upungufu na kuwatangazia waombaji husika kwa ajili ya kurekebisha kasoro zilizojitokeza.

Mkurugenzi huyo aliwataka wazazi, walezi na wanafunzi kuendelea kufuatilia vyanzo rasmi, ikiwamo tovuti ya HESLB (www.heslb.go.tz), kuhusu taarifa muhimu na orodha ya watakaopangiwa mikopo kwa mwaka wa masomo 2020/21, kwa mujibu wa kalenda ya mwaka wa kitaaluma ya mwaka huu.

Serikali kupitia HESLB, imetenga Sh. Bilioni 464 kwa ajili ya wanafunzi 145,000 katika mwaka wa masomo wa 2020/21.

Kati yao, wanafunzi wanufaika 54,000 watakuwa wa mwaka wa kwanza na 91,000 ni wanafunzi wanaoendelea na masomo.

# Abiria 22 wajeruhiwa ajali ya basi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WATU 22 wamejeruhiwa baada ya basi walilokuwa wakisafiria kutoka Mbeya kwenda Mwanza, kuacha njia na kupinduka katika eneo la Inyala, nje kidogo ya jiji, huku wanane kati yao wakiwa katika hali mbaya.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) Ulrich Matei, alisema basi lililohusika katika ajali hiyo ni la kampuni ya Isamilo lenye namba za usajili T.629 CQC.

Alisema ajali hiyo ilitokea jana saa 12:40 asubuhi wakati likitokea jijini Mbeya umbali wa kilomita 20 kutoka kituo kikuu cha mabasi.

Matei alisema chanzo cha ajali hiyo ni uzembe wa dereva, Kini Malimi (51) mkazi wa Igoma jijini Mwanza ambaye alitaka kuyapita magari mengine yaliyokuwa mbele yake bila kuchukua tahadhari.

Mbali na kutaka kuyapita magari hayo, alisema pia dereva huyo alikuwa anaendesha gari kwa mwendokasi mkubwa, hivyo akashindwa kulimudu na hivyo likapinduka.

"Watu hao wamepata majeraha sehemu mbalimbali za miili yao. 12 kati yao ni wanaume na 10 ni wanawake lakini majeruhi wanane wamekimbizwa katika Hospitali ya Rufani Kanda ya Mbeya na wengine 14 wanaendelea na matibabu katika Kituo cha Afya Inyala," alisema Kamanda Matei.

Alisema mbali na abiria hao kujeruhiwa pia kulitokea na uharibifu wa mali mbalimbali zikiwamo za abiria pamoja na gari lenyewe ambalo lilipasuka vioo.

Matei aliwataka madereva wa vyombo vya moto kufuata sheria za usalama barabarani ili kuepusha madhara kama yaliyotokea kwenye gari hilo, huku akiwataka abiria kuwadhibiti madereva wanaoendesha magari kwa mwendo mkali.

# EU yaombwa kuondoa vizuizi vya kusafiri

**Na Mwandishi Wetu**

JUMUIYA ya nchi za Afrika, Carribean na Pacific (OACPS) imetoa wito kwa Umoja wa Ulaya kuondoa vizuizi vya kusafiri kwa baadhi ya nchi hususan zile zilizoonyesha kuwa salama zaidi dhidi ya maambukizi ya corona kama Tanzania.

Taarifa iliyotolewa jana na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, ilisema wito huo ulitolewa katika kikao maalum cha mashauriano baina ya nchi wanachama wa OACPS na Ujerumani ambayo kwa sasa ni Rais wa Baraza la Umoja wa Ulaya.

Mashauriano hayo yaliyofanyika juzi katika Ofisi za Jumuiya ya OACPS, Brussels, Ubelgiji, yaliongozwa na Balozi wa Tanzania nchini Ubelgiji na Mwakilishi wa Tanzania katika Umoja wa Ulaya ambaye ni Mwenyekiti wa mabalozi wa nchi za OACPS walioko Brussels, Jestas Nyamanga na ujumbe wa Ujerumani uliongozwa na Waziri wa Masuala ya Ushirikiano wa Uchumi na Maendeleo wa Serikali ya Shirikisho la Ujerumani, Dk. Gerd Mùller.

Katika kikao hicho, taarifa hiyo ilisema wajumbe walisisitiza umuhimu wa Umoja wa Ulaya (EU) kuendelea kuunga mkono Shirika la Afya Duniani (WHO) katika kusimamia ithibati za utafiti wa chanjo za ugonjwa wa corona na shirika hilo kuendelea kujengewa uwezo wa kusimamia utaratibu wa kuhakikisha kuwa chanjo itakayothibitika inawafikia mataifa yote kwa usawa na kwa gharama nafuu.

Kikao hicho kilijadili pia hatua mbalimbali zinazopaswa kuongeza msukumo kwa EU katika kuzisaidia nchi za OACPS kukabiliana na athari za kiuchumi zinazotokana na corona hususan katika sekta za utalii na kilimo.

Mikakati iliyojadiliwa ni pamoja na ile inayolenga kupunguza, kufuta au kubadilisha masharti ya ulipaji wa madeni ya nchi za OACPS na wito wa nchi hizo kuitaka EU kusogeza mbele utekelezaji wa baadhi ya kanuni na taratibu mpya za biashara zilizopangwa kuanza kutumika mwanzoni mwa mwaka ujao.

Kupitia mashauriano hayo, taarifa ilisema, pande zote mbili zilitathmini mwenendo wa majadiliano ya mkataba mpya wa ubia wa ushirikiano wa kiuchumi baina ya OACPS na EU yanayoendelea hivi sasa baada ya mkataba wa sasa kufikia kikomo Desemba, mwaka huu.

Pande hizo zilijadili kwa kina namna ya kushirikiana katika maeneo yanayolenga kuongeza mnyororo wa thamani ya mazao ya kilimo, uwiano ulio sawa katika biashara na maendeleo ya teknolojia katika kukuza uchumi na maendeleo ya watu.

Kikao kilihitimishwa kwa Ujerumani kuonyesha utayari wa kuyapa kipaumbele masuala yote yaliyojadiliwa katika kipindi cha uongozi wake wa Baraza la EU na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki katika kipindi hiki ambacho inashika nafasi ya Rais wa Baraza la Mawaziri wa nchi 79 wanachama wa OACPS.



Kazi ya ujenzi wa daraja kubwa katika barabara ya Shekilango eneo la Legho ikiendelea jijini Dar es Salaam jana, ambapo likikamilika huenda likamaliza kero ya maji kujaa na kupita juu wakati wa msimu wa mvua na kusababisha mawasiliano ya barabara kukatika. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Ushahidi kesi mchungaji madai ya ubakaji waanza kushika kasi

**Na Julieth Mkireri,** CHALINZE

KESI ya ubakaji inayomkabili Mchungaji wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri (KKKT) Dayosisi ya Morogoro, Jimbo la Chalinze, Boniface Mgalula, imeendelea kusikilizwa katika Mahakama ya Mwanzo Lugoba mkoani Pwani.

Katika kesi hiyo ambayo inasikilizwa na Hakimu Vedastus Mwaria, mashahidi watatu wa upande wa Jamhuri wameanza kutoa ushahidi wao.

Shahidi wa kwanza, Gift Moses, juzi alidai mahakamani hapo kuwa aliona hali ya tofauti ikiwa ni pamoja na mabadiliko ya kimwili kutoka kwa mdogo wake (jina linahifadhiwa).

Kutokana na hali hiyo, alidai kuwa aliamua kumhoji ndipo alipokiri kuwa ni mjamzito na kwamba aliogopa kuwaeleza familia yake hali hiyo kutokana na vitisho kutoka kwa mtuhumiwa.

Moses alidai kuwa baada ya kumaliza kuzungumza na mdogo wake, alilazimika kumpigia simu mama wa binti ambaye alikuwa masomoni mkoani Kilimanjaro na kumweleza kuwa binti yake ana ujauzito.

Shahidi wa pili, Rehema Peter, alidai kuwa taarifa za binti huyo kuwa mjauzito alizipata kutoka kwa mtoto wa wifi yake, Gift Moses, na baada ya hapo alimpigia simu mume wake, Peter Ndongo, kumwelezea taarifa hizo.

Rehema alidai mahakamani hapo kuwa Juni 13, mwaka huu, alipata taarifa hizo na kumpigia mume wake ili azifanyie kazi kwa kuwa yeye ndiye aliyebaki na watoto. Pia alidai kuwa Mchungaji Mgalula, ambaye ni mtuhumiwa, alimpigia simu kumuuliza kama kuna taarifa yoyote aliyoipata kutoka nyumbani kwake na taarifa hizo mumewe amemshirikisha nani mwingine kwani amepigiwa simu na Katibu wa Usharika akimtaka wakutane.

Shahidi huyo aliendelea kudai kuwa mtuhumiwa alimpigia simu kwa mara nyingine Juni 18, mwaka huu, saa 11:00 alfajiri na kumhoji kwa nini mume wake amechukua uamuzi wa kulifikisha suala hilo kwa wazee badala ya kumwita wayamalize.

Naye Peter Ndongo, shahidi mwingine katika kesi hiyo, alidai mahakamani kuwa baada ya kupokea simu kutoka kwa mke wake, iliyompatia taarifa za ujauzito wa mwanawe, aliamua kukaa kuongea naye ndipo alipokiri kuwa taarifa hizo ni za kweli.

Alidai baada ya hapo, hatua aliyochukua ni kuripoti polisi na baadaye kwenda hospitalini kumpima binti huyo ambaye aligundulika na ujauzito wa wiki 30.

Ndongo aliiambia Mahakama kwamba binti yake alimweleza kuwa ujauzito huo ni wa chungaji Boniface Mgalula na alimbaka Januari 6, mwaka huu, baada ya kumwita akitoka kuzima taa kanisani.

Shahidi alidai kuwa binti huyo alimwambia kuwa mtuhumiwa baada ya kumwita ndani, alimbaka kwenye korido la nyumba yake na kisha kumtishia endapo atatoa taarifa za kitendo hicho atamuua na kumfukuza kazi baba yake ambaye ni mwinjilisti katika kanisa hilo.

## Watumiaji M-Pesa wapata gawio bil. 3.5/-

**Na Mary Geofrey**

WATUMIAJI wa huduma ya Vodacom M-Pesa, milioni 8, wamepata gawio la faida ya Sh. bilioni 3.5 kutoka kwenye akaunti ya M-Pesa Trust.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, Mkurugenzi wa M-Commerce, Epimack Mbeteni, alisema gawio hilo limeanza kutolewa kwa wateja hao wa M-Pesa kuanzia jana.

"Tunashauku ya kugawana faida hii na wateja wetu kwani wao ndio sababu ya mafanikio ya huduma ya M-Pesa. Huduma ya M-Pesa imechangia maendeleo ya Watanzania na mpango huu umedhamiria kuendelea kuwapa wateja wetu faida zaidi," alisema Mbeteni.

Alisema wateja wote wa Vodacom ambao wamekuwa wakitumia M-Pesa kuanzia Januari Mosi hadi Machi 31, mwaka huu, watafaidika na bonus hiyo ya Sh. bilioni 3.5 ambayo itagawiwa moja kwa moja kupitia M-Pesa.

Alisema kuanzia sasa wateja wa Vodacom wataweza kutuma SMS ya neno KIASI kwenda namba 15300, ili kujua kiwango gani cha faida watapokea.

Mbeteni alisema, baada ya kupata gawio hilo, wateja wa M-Pesa wanaweza kukomboa faida hiyo kwa kuitoa kama fedha taslimu, kununua muda wa maongezi, vifurushi au kulipia bili.

"Kiasi ambacho mtu atapokea kama sehemu ya faida hiyo itategemea na idadi ya miamala aliyokuwa akifanya kwa kipindi nilichotaja hapo juu," alisisitiza Mbeteni.

Alisema hadi sasa Vodacom imeshagawa faida ya jumla ya Sh. bilioni 133 kwa wateja wa M-Pesa.

# Wakazi Dar wazingirwa na majitaka kwa miezi 4

**Na Mwandishi Wetu**

WAKAZI wa eneo la Makumbusho Mtaa wa Kijitonyama Bwawani wamezingirwa na majitaka yenye kinyesi kwa zaidi ya miezi minne sasa, huku mamlaka zinazohusika zikiwa hazijachukua hatua za kuyaondoa.

Wakizungumza na gazeti hili jana, baadhi ya wakazi wa mitaa ya Tanzania, Soweto na Mali eneo la Makumbusho walisema wamekuwa wakiishi kwa kuzingirwa na maji hayo kwa muda wote, kutokana na kuharibika kwa mfumo wa majitaka kwenye eneo hilo.

Mmoja wa wakazi hao ambaye pia alikuwa Mwenyekiti wa ujenzi wa mfumo wa majitaka mwaka 1998, Dennis Kessy, alisema hali hiyo imekuwa kero, kutokana na mfumo wa majitaka uliopo kuzidiwa na kuharibika, hivyo maji kurudi kwenye makazi ya watu.

Alisema mfumo wa majitaka kwenye eneo hilo ulikuwa maalum kwa ajili ya makazi ya watu wa zilizokuwa nyumba za Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) ambao walichangia Sh. 90000 kila nyumba kwa ajili ya jenzi wa mfumo huo mwaka 1998, ambao sasa umezidiwa kutokana na ongezeko la majengo.

"Wakati mfumo huo unajengwa na wananchi kwa kushirikiana na Irish Aid, hakukuwa na maghorofa, lakini sasa hivi kuna maghorofa karibu na eneo la nyumba za zamani ambazo zote zinategemea mfumo huo huo ambao ulitengenezwa kuhudumia watu wachache."

"Mfumo huo ulikuwa maalum kwa ajili ya kupokea maji machafu kutoka kwenye makazi yetu na kuyapeleka moja kwa moja baharini... kwa hiyo sisi hatukulazimika kujenga makaro. Lakini zaidi mabomba yaliyotumika yalikuwa yenye uwezo wa kubeba mzigo wa wakati ule," alisema Kessy.

Alisema mfumo huo wa majitaka ulipoharibika maji hayo machafu yamekuwa yakitapakaa kwenye makazi ya watu na hata baada ya kutoa taarifa kwa DAWASA hakuna hatua zozote zilizochukuliwa.

Angela Mganga, alisema ameishi hapo toka mwaka 1974, lakini hajawahi kushuhudia kero ya aina hiyo, ambayo imemlazimisha kuhamisha familia yake na kuwapeleka kwa ndugu zake.

Alisema nyumba yake iliyoko Mtaa wa Tanzania ni kati ya nyumba zilizozingirwa na maji ya kinyesi muda wote, huku akiwa hajui la kufanya.

"Tatizo hili tulilipeka serikali ya mtaa kuomba msaada na pia tumekwenda hadi DAWASA wilaya wakati tatizo hili linaanza, lakini hakuna hatua yoyote iliyochukuliwa," alisema.

Felicianus Kamukara, Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Kijitonyama Bwawani, alisema alichukua hatua kadhaa ikiwamo za kuwasiliana na DAWASA, kwa kuwa tatizo hilo lipo katika eneo kubwa kwenye Kata ya Kijitonyama, lakini hakuna kilichofanyika. Alisema kwa maelezo ya wataalamu, alijaribu kuzunguma nao na kuelezwa tatizo lipo kwenye makutano ya barabara ya Sayansi ambapo eneo hilo linadaiwa kutitia, hivyo kuathiri mfumo wa mabomba ya majitaka yanayokwenda kumwaga maji hayo baharini.

'Ni kweli tatizo hili ni kubwa ni karibu miezi mitano sasa haya maji yenye vinyesi hayaendi popote, na yamekwama kwenye maeneo ya makazi. Nimefika hadi kwa Mkuu wa Wilaya, lakini halijapatiwa ufumbuzi," alisema Kamukara. Ofisa Habari wa DAWASA, Evalasting Lyaro, alisema ofisi yake haina taarifa za tatizo hilo, lakini hata hivyo atafuatilia ili kujua undani wake.



Mkazi wa Mtaa wa Bwawani, eneo la Makumbusho, Kata ya Kijitonyama, jijini Dar es Salaam, akionyesha kwa waandishi wa habari jana, majitaka yaliyozingira moja ya nyumba zilizopo kwenye eneo hilo, kwa zaidi ya miezi minne sasa na kusababisha kero kubwa kwa wakazi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kagera washauriwa tahadhari mvua za vuli

**Na Lilian Lugakingira,**
BUKOBA

WAKAZI wa Mkoa wa Kagera wametakiwa kuchukua tahadhari katika msimu huu wa mvua za vuli ulioanza wiki ya pili ya Septemba, ili kuepuka madhara yanayoweza kuwakumba.

Miongoni mwa madhara hayo ni mafuriko, ambayo husababisha vifo na uharibifu wa mali na mazao.

Aliyetoa angalizo hilo ni Meneja wa Mamlaka ya Hali ya Hewa (TMA) Mkoa wa Kagera, Stephen Malundo, kwa kusema utabiri wa sasa unaonyesha mvua katika mkoa wa Kagera zitanyesha za wastani au chini ya wastani.

"Lakini hii isiwe sababu ya wananchi kutochukua tahadhari, maana kunaweza kujitokeza vipindi vya mvua kubwa na kuleta madhara, kwa hiyo kuweni makini hadi mwisho wa msimu Januari 2021," alisema.

Alitaja baadhi ya miezi na kiwango cha mvua kinachotarajiwa kutokana na utabiri huo kuwa Oktoba ni wastani wa milimita 158, Novemba ni wastani wa milimita 204 na Desemba wastani wa milimita 181, na kuwa jumla ya msimu mzima wa vuli wanatarajia itakuwa ni wastani wa milimita 544 au chini ya hapo.

"Kwa utabiri huu ina maana kuna maeneo mengine yatakuwa na mvua za chini ya wastani na mengine yatakuwa na mvua za wastani, kwa hiyo wananchi watakaokuwa maeneo yenye mvua chini ya kiwango ni vizuri wakalime mazao yanayokomaa kwa muda mfupi na yanayovumilia unyevu mdogo kama viazi vitamu ili kujinusuru kukumbwa na baa la njaa," alisema.

Aidha, aliwataka wakulima kuonana na maofisa ugani ili kupewa maelekezo sahihi ya mazao gani au mbegu gani wapande kulingana na maeneo walipo, na kuwa inatarajiwa mvua hizo za vuli zitakwisha Januari 2021.

Mmoja wa wananchi waliozungumza na Nipashe, Pastory Anathory, alisema wameshaandaa mashamba na kuwa walikuwa wakisubiri mvua ili waaanze kupanga.

"Kama tunaambiwa mvua zitakuwa za wastani au chini ya wastani, basi tumuombe Mungu atuvushe salama, maana hatuna uwezo wa kulima kilimo cha umwagiliaji," alisema.

Jumanne wiki hii, wakulima nchini walishauriwa kulima mazao yanayostahimili ukame kutokana na upungufu mkubwa wa mvua unaotarajiwa kutokea katika kipindi cha mvua za vuli nchini.

TMA ilisema katika kipindi cha mvua hizo za mwezi Oktoba, Novemba na Desemba (OND) mikoa mingi itakuwa na upungufu mkubwa wa mvua.

Mkurugenzi Mkuu wa TMA, Dk. Agnes Kijazi, alisema mifumo ya hali ya hewa inaonyesha kutakuwa na mvua ndogo kufika chini ya watani kwenye mikoa ya Dar es Salaam, Zanzibar, baadhi ya maeneo ya mkoa wa Morogoro, Arusha, Kilimanjaro, Manyara, Tanga, Simiyu, Mwanza, Shinyanga, Geita, Kagera, Mara na baadhi ya meneo ya mkoa wa Kigoma.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Uhamasishaji umma ukomeshe hujuma hizi

**TABIA** ya baadhi ya wanajamii kuhujumu miundombinu mbalimbali ikiwamo ya maji ni miongoni mwa mambo ambayo hufanyika kwenye maeneo mengi ya miji na majiji pamoja na Dar es Salaam.

Hujuma hizo husababisha wengine kukosa huduma hiyo kutokana na uharibifu.

Mtindo huo kwa namna moja ama nyingine unaweza kuwa mojawapo ya kikwazo cha maendeleo, hivyo kila Mtanzania kwenye eneo lake hana budi kuchukua hatua anapoona hujuma inafanyika.

Kuna mifano mingi ya hujuma hizo, lakini mmojawapo ni ya baadhi ya watu wanapoona bomba la maji ya kunywa limepasuka, badala ya kutoa taarifa kwa mamlaka husika, kama DAWASA kwa Dar es Salaam, wanafurahia na kushangilia kwa kubeba misururu ya ndoo na madumu na kuhamia eneo lilipasuka ili kuchota maji.

Wapo wengine wanaolipasua zaidi iwe ni kulikata au kulichimba bomba hilo ili kupata maji ya kutosha.

Tabia hiyo haitofautishwi na kuharibu miundombinu mingine kama kung'oa alama za barabarani , kubomoa vyuma vya madaraja na hata kujiunganishia umeme kwa kutumia vishoka.

Tunaona kuwa kuna haja ya kuwafundisha wananchi na kuwahamasisha kuwa wazalendo kwa nchi yao, kulinda maendeleo yaliyopo na yajayo kwa faida ya sasa na ijayo kuliko kudhani kwamba ni jambo la kawaida kuharibu na kuvuruga kazi za maendeleo zilizofanyika.

Tunashauri katika mikutano ya hadhara hasa nyakati za kampeni iwe jukwaa la kuwahamasisha wananchi kupenda na kulinda mali ya umma maana hata wao ni sehemu ya uwekezaji huo kwa vile wanalipa kodi, kushiriki kazi za maendeleo kwa kujitolea nguvu zao hivyo ni vyema wakathamini na kujiona kuwa kuhujumu kazi hizo ni kujishambulia.

Ni vyema wakahamasishwa kuwa kisingizio cha ugumu wa maisha kisiwe sababu ya baadhi ya watu kujihusisha na hujuma hizo na pia wafahamu kuwa wamefikia katika hatua ya kukosa baadhi ya huduma muhimu kutokana na baadhi ya watendaji kuhujumu na rasilimali za nchi na kutumia fedha za maendeleo kwa manufaa binafsi.

Wanaofanya hujuma hizo wakielimishwa ama kuchukuliwa hatua za kisheria na jamii hasa polisi jamii itakuwa ni njia mojawapo ya kukomesha mtindo huo ambao ni kama umezoeleka .


Licha ya kwamba kuna tatizo la ukosefu wa maji kwenye baadhi ya maeneo ya miji na maji tunaona kuwa haitoshi kuwa sababu ya kuhujumu rasilimali hasa pale mabomba yanapopasuka.

Ni wakati wa kila mmoja kuwa mlinzi wa miundombinu kwenye eneo analoishi ili kumaliza matatizo ya hujuma ambayo yanalenga kukwamisha maendeleo kwa vile wizi huo hufanyika sehemu nyingi za nchi kuanzia kwenye barabara, reli na maeneo mengine hali ambayo haina budi kukomeshwa.

Hata hivyo, pamoja na kuhamasisha mabadiliko mamlaka za kusimamia maji zinawajibika kuwa na ufuatiliaji na ulinzi wa miundombinu ya huduma hiyo kwa kuwa upotevu wa maji sehemu nyingi ni tatizo lisilokwisha.

Wakati mwingine tunaweza kushawishika kuwa kiasi cha maji yanayopotea njiani ni kikubwa kuliko yale yanayowafikia wateja Ni kwa msingi huo tunashauri kuwa wenye mtindo huo hasa wafanyabiashara wa maji maeneo yasiyo na maji safi na salama wabadilike na kutambua kuwa ndiyo walinzi wa kwanza na wawe tayari kutoa taarifa za aina zote za hujuma ama uharibifu ili hatua stahiki zichukuliwe haraka.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Jenifer Gilla

## Muungwana Lazima Nilonge

# Uwekezaji kukabili ukame uanze sasa

**UTAALAMU** asilia na wa kisasa unahitajika kukabili ukame utakaoikabili mikoa ya Arusha, Manyara, Kilimanjaro, Tanga, Zanzibar na Pemba wakati wowote kuanzia sasa.

Kwa mujibu wa utabiri wa Mamlaka ya Hali ya Hewa (TMA), mikoa hiyo na ukanda wa pwani ijiandae kwa ukame bila mvua za vuli.

Ni wazi kuwa vijiji vingi vya maeneo hayo vitatikiswa na ukame utokaochangiwa na jua kali na upepo ambao kwa maelezo ya TMA utakausha maji, kuumiza mazao, kudhoofisha tabaka la mboji la ardhi.

Hata hivyo, ukame huo ambao sababu mojawapo ni mabadiliko ya tabianchi, haukwepeki unaendelea kutishia, kukausha vyanzo vya maji na kudhoofisha rutuba ya ardhi kutokana na upepo hasa kipindi hiki mvua zinapopotea kwa muda mrefu.

Huo ndiyo mtihani kwa jamii nyingi za mikoa ya Kilimanjaro, Tanga, Arusha, Manyara, Dar pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba.

Ndiyo maana ni wakati wa kutumia mbinu mpya au za kisasa kwa kuzichanganya na zile za asili za kitamaduni kudhibiti ukame. Wapo wanavijiji wanaofahamu namna bora ya kutunza vyanzo hivyo kwa kutumia mbinu za asili na utaalamu wa kijadi.

Mbinu hizo ni kama za kuhifadhi maji na rutuba ya ardhi au hata kuvuta maji yanayozama ardhini kutokana na ukame.

Kwenye mikoa hiyo vijiji na sehemu nyingi zina uoto wa kijani unaohifadhi vyanzo vya mito, ardhi oevu na misitu. Cha msingi ni wananchi wajitahidi kupanda miti kutunza mazingira hayo pamoja na kuhifadhi maji.

Baadhi ya maeneo ya miti maarufu kutunza na kuvuta maji yaliyo ardhini kwa mfano mikuyu, mivumo, mianzi na jamii ya matete na masale.

Ni vyema kuanzia sasa wananchi wakapanda mimea na miti kama mikuyu na mivumo kutunza vyanzo hivyo na kusaidia kuvuta maji yanayozama ardhin i kutokana na ukame.

Wananchi pamoja na kuhifadhi mazingira wasisitizwe kupanda miti ya asili ili kutunza uoto wa asili na inapokutisha majani yanabaki kuwa mbolea.

Wataalamu wa mazingira wanaeleza kuwa miti ya asili inazalisha mboji na matunda yake ni mbolea bora ikilinganishwa na ya kigeni.

Miti kama maparachichi, mafenesi au mapera licha ya kuwa ni mazao ya biashara yanayoleta fedha kwani matunda yake yana soko, yanatajwa kuharibu ardhi kwa kukausha maji ndani ya mwamba ulio karibu.

Kadhalika, hata majani yake yanayodondoka si rafiki wa mkulima. Ni makavu, hayazalishi rutuba ya mboji, lakini baya zaidi huzuia uoto mwingine kustawi hasa mazao ya chakula, biashara na nyasi za asili.

Mfano halisi ni maparachichi ambayo yanatajwa na wanavijiji kuwa licha ya kuangusha majani mengi ni makavu, hayachanganyikana na ardhi kutengeneza mboji na rutuba.

Mara nyingi majani haya hayaozi, muda wote ni makavu na hata kama mvua ikinyesha yanachukua muda mrefu kujishindilia ardhini, kuoza na kuwa vigumu kuchanganyikana na udongo.

Taarifa za ukame zinapotolewa na TMA ni wakati pia wa kuhifadhi maji kwa juhudi zaidi ikiwamo kutumia mbinu za asilia kama kuchimba na kukijengea chanzo, kukizungushia ukuta wa masale, mikuyu na mivumo na mimea inayohifadhi maji.

Wataalamu wa mazingira ya asili na uhifadhi ardhi wanasema inatunza maji hata kama jua na upepo vitakuwa vikali.

Ni kwa mtizamo huu kwamba wadau na serikali washirikiane na wananchi kuchanganya mbinu za jadi za kisasa na taarifa za kitafiti na teknolojia ya kisasa kuhifadhi maji na kutunza mazingira, ili kukabiliana na ukame unaotokana na ongezeko la joto na uharibifu wa mazingira.

Habari ya kupanda miti au kampeni za panda mti kata mti ziangalie pia uelewa wa kiasili walio nao Watanzania wa vijijini kwani kuna hazina kubwa ya ufahamu iliyo ndani ya utamaduni wa kila kabila.

Wataalamu wasaidie kusambaza mikuyu pengine na kutafiti iwapo inaweza kustawi mikoa mikame zaidi kama Dodoma, Singida, Tabora na Shinyanga.

Tena, badala ya kupanda mikaratusi, mikenge, miarobaini na mikurunge mijini, serikali ihimize upandaji wa miti ya asili.

# HEKA HEKA KAMPENI ZA UCHAGUZI MKUU



Mgombea ubunge wa Jimbo la Mbeya Mjini kwa tiketi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dk. Tulia Ackson, akiwahutubia wananchi wa Jiji la Mbeya juzi, wakati wa uzinduzi wa kampeni za ubunge kwenye jimbo hilo uliofanyika kwenye uwanja wa CCM Ruanda Nzovwe jijini humo. **PICHA: NEBART MSOKWA**



Mjumbe wa Kamati Tendaji ya Baraza la Wanawake la Chama cha Demokrasia na Maendeleo (BAWACHA) Wilaya na Mwenyekiti wa baraza hilo, Kata ya Temi, Grace Rukwembe, akiomwombea kura mgombea udiwani wa Kata ya Kimandolu, Erick Ole Tunga (hayupo pichani), katika uzinduzi wa kampeni kwa kata hiyo, jijini Arusha mapema wiki hii. **PICHA: DANIEL SABUNI**



Mgombea ubunge wa Jimbo la Dodoma Mjini kwa tiketi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Anthony Mavunde, akimnadi mgombea udiwani wa Kata ya Nala, Julius Chimombo, katika mkutano wa kampeni za uchaguzi mkuu, jimboni huo. **PICHA: AUGUSTA NJOJI**



Mgombea ubunge Jimbo la Shinyanga Mjini, kupitia Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Salome Makamba, akijinadi kwa wananchi wakati wa mkutano wa kampeni za uchaguzi mkuu uliofanyika jimboni humo mapema wiki hii. **PICHA: MARCO MADUHU**



Wakereketwa na wanachama wa Chama cha Wananchi (CUF) Wilaya ya Masasi mkoani Mtwara wakimshangalia mgombea ubunge wa chama hicho, Jimbo la Masasi Mjini, Hamza Machuma (katikati), baada ya kumaliza kuhutubia mkutano wa hadhara wa kampeni za uchaguzi mkuu katika viwanja vya Mti Mwiba mjini Masasi juzi. **PICHA: HAMISI NASRI**



Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Wazazi ya CCM, Erasto Sima (kushoto), akimnadi mgombea ubunge Jimbo la Ilala, Mussa Azzan Zungu, wakati wa mkutano wa uzinduzi wa kampeni katika jimbo hilo, jijini Dar es Salaam. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Wakulima wakunwa kupelekewa matrekta

**Na Mwandishi Wetu,**
SUMBAWANGA

WAKULIMA wa mahindi mkoani Rukwa wamesifu mpango wa kupelekewa matrekta na mafunzo na kusema kuwa mpango huo unakuza uwezekano wa wakulima kuuza mahindi na vyakula vingine Zambia na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC).

Mpango wa kupeleka matrekta kwa wanachama wa vyama vya msingi vya ushirika, ni kati ya Kampuni ya AGRICOM Africa Limited, uongozi wa mkoa na vyama vikuu vya ushirika. Kampuni ya AGRICOM inaendesha mafunzo kwa viongozi na wanachama wa ushirika kabla ya vyama kukopeshwa zana hizo.

Mwenyekiti wa Malagano AMCOS, Norbert Sikombe, alisema Mkoa wa Rukwa una uhaba mkubwa wa matrekta na kwamba hayo machache hayatoshi kuwakodisha wakulima.

Programu hii ikifanikiwa mkoa utakua na matrekta ya kutosha na wanachama wa vyama vya ushirika watalima mashamba yao wakati muafaka.

"Naipongeza Serikali ya Mkoa, Kampuni ya AGRICOM na vyama vyama vya ushirika kuliona hili. Kazi ikienda vizuri tutanuafaika,|" alieleza Sikombe.

Mwanachama wa AMCOS hiyo, Gasper Mpepo, alisema vyakula vinavyozalishwa Tanzania, hasa mahindi, vina soko Zambia na DRC. "Soko lipo ndani na nje. Tunachohitaji ni zana bora kuzalisha kwa wingi ili tuwapelekee wateja mazao watupe fedha ili tubadilishe maisha yetu," alisema na kukumbusha kwamba kijiji chao ndicho kinazalisha kwa wingi mahindi mkoani Rukwa.

Wakazi kadhaa wa Mkoa wa Rukwa hufanyabiashara Zambia na DRC. Wanaughaibuni kutoka Rukwa wanaishi Zambia (asilimia 67) na DRC asilimia 17.

Mwanakikundi cha Chipukili, Daud Sungura, alisema mafunzo yanayotangulia uboreshaji wa zana ni muhimu maana wanavijiji wamezoea kutumia majembe. "Tukipata zana hizo na mafunzo ya kuzitumia vizuri, tutapiga hatua," alieleza.

Kaimu Meneja Mkuu wa Kampuni ya AGRICOM, Remmy Nindi, alisema kampuni yao imedhamiria kutekeleza mpango huo ili kuinua kilimo cha mahindi mkoani humo.

Vyama vitakavyopata matrekta, pamoja na masharti na vigezo vingine, ni kuwa na wanachama wasiopungua 72 na kudhihirisha uwezo wa kifedha wa kununua matrekta hayo kwa mkopo.

Kampuni ya AGRICOM imeingia katika makubaliano hayo kama wa mdau kutoka sekta binafsi katika kutekeleza mpango wa kuinua kilimo nchini wa ASDP II.

# Mgombea mwenza CUF ajinasibu kusimamia madeni ya wakulima

**Na Stevie Chindiye**,
TUNDURU

MGOMBEA mwenza wa urais wa Chama cha Wananchi (CUF), Hamida Abdalah, amesema endapo chama chake kitapata ridhaa kuingia madarakani, kitasimamia na kuhakikisha fedha za wakulima zinalipwa kwa wakati.

Hamida ambaye chama chake kimemsimamisha Prof. Ibrahim Lipumba kugombea urais, amesema mkazo mkubwa utakuwa kwa wakulima wa korosho, mbaazi na ufuta katika mikoa ya kusini.

Alitoa ahadi hiyo juzi wakazi wa mikutano ya kampeni ya chama hicho aliyoifanya kwa nyakati tofauti katika Kijiji cha Lukumbule na kwenye viwanja vya Baraza la Idd, mjini hapa.

Pia alisema chama hicho kimeandaa Ilani ambayo inazungumzia kuleta maendeleo katika nyanja za afya kwa koongeza dawa ili kuwapunguzia adha wanawake wa vijijini na kuboresha miundombinu ya barabara na maji.

Katika mikutano hiyo, mgombea huyo aliwanadi madiwani na mgombea ubunge kwa tiketi ya CUF katika jimbo la Tunduru Kusini, Mariam Pillah. Pia alisema chama kinafuatilia rufani ya mgombea ubunge katika jimbo la Tunduru Kaskazini, Ally Mandunda.

Awali, Mwenyekiti CUF Kata ya Majengo, Mohammed Alifa na Mwenyekiti wa CUF Wilaya ya Tunduru, Hussein Komba, walimweleza mgombea mwenza huyo kuwa kuna taarifa kutoka kwa wakulima wa wilaya hiyo kuwa wamekuwa wakiuza mazao yao kwa mfumo wa stakabadhi ghalani kwa bei ndogo huku wakikopwa.

Walisema wakati wakulima wamekuwa wakiuza mazao yao kwa kukopwa, wenzao katika wilaya jirani wamekuwa wakiuza kwa fedha taslimu na kujipatia stahiki zao kwa wakati.

Pamoja na kukopwa, walisema wamekuwa wakikatwa mchango wa Sh. 70 kwa kila kilo moja ili kuchangia timu ya mpira na mchango wa lazima wa Sh. 30 kwa kila kilo kuchangia elimu bila ridhaa yao wakati serikali inatoa elimu bure.



Mwanafunzi akipita jirani na taka zilizotelekezwa kwa muda mrefu kando ya ukuta, katika eneo la Lufungila, Mtaa wa Mlalakua, jijini Dar es Salaam jana, kitendo ambacho ni hatari kwa afya za wakazi wa eneo hilo. **PICHA: FLORIDA RAYMOND-TUDARCo**

# Vibali ununuaji misitu sasa miaka mitatu

**Na Francis Godwin,**
MAFINGA

WAKALA wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) na wavunaji wa miti, wameingia makubaliano mapya ya miaka mitatu ya uvuaji miti katika misitu ya serikali kote nchini.

Akizungumza jana wakati wa hafla fupi ya kutia saini makubaliano hayo iliyofanyika katika ukumbi wa TFS mjini hapa, Kamishana Mkuu wa Uhifadhi wa TFS, Prof. Dos Santos Silayo, alisema utaratibu huo ni mpya.

Alisema awali TFS ilikuwa ikiingia makubaliano ya mwaka mmoja mmoja na wavunaji hao ila sasa wameongeza muda ili kuwawezesha wavunaji kupata fursa ya mikopo katika taasisi za kifedha.

Prof. Silayo alisema kwa sasa wanaondoka katika utaratibu wa awali wa wavunaji kupata vibali vya mwaka mmoja wa kupata mali ghafi katika misitu ya serikali nchini.

Alisema kilio cha wavunaji kilikuwa kikubwa hasa kukosa mikopo katika taasisi za fedha kutokana na muda wa mwaka mmoja ambao walikuwa wakipewa mikataba ya kupata mali ghafi katika misitu hiyo.

Ili kuhakikisha wavunaji hao wananufaika na utaratibu huo mpya, alisema tayari taasisi mbalimbali za fedha zimesha jitokeza kuonyesha nia ya kuwasaidia mikopo wavunaji hao. Prof. Silayo alisema katika kipindi cha miaka takribani mitano sasa, kumekuwa na ongezeko kubwa la viwanda nchini, vikiwamo vya uchakataji wa mazao ya misitu, lakini hawajivunii zaidi ongezeko la viwanda bali ukuaji wa teknolojia mpya.

Alisema sasa wenye viwanda wanayo teknolojia ya kisasa ambayo inaweza kuchakata kuanzia karatasi hadi mkaa mbadala jambo ambalo ni la kujivunia katika ukuaji wa teknolojia ya mitambo ya uchakataji wa mazao ya misitu.

Pia alisema jitihada mbalimbali zilizofanywa na serikali kupitia TFS zimeongeza idadi kubwa ya wafanyabiashara kuwekeza katika sekta ya viwanda vya uchakataji wa mazao ya misitu na kuanza kuzalisha bidhaa mbalimbali ambazo awali taifa lilikuwa likiagiza toka nje ya nchi.

Kamishna huyo alisema miaka ya nyuma, Taifa lilikuwa likiagiza nguzo za umeme kutoka nje ya nchi, lakini kwa sasa baada ya wawekezaji wa ndani na wale wa nje kuwekeza katika viwanda vya mazao ya misitu, sasa nguzo zinazalishwa ndani kupitia malighafi zinazopatikana katika misitu ya serikali.

Mkuu wa Wilaya ya Mufindi, Jamhuri William, ambaye alikuwa mgeni rasmi katika hafla hiyo, mbali na kupongeza hatua kubwa iliyofikiwa na TFS ya kuzindua uratatibu mpya wa kuingia mikakata ya miaka mitatu na wavunaji hao, alisema bado serikali haiko tayari kuona kuna sekta yenye changamoto zisizofanyiwa kazi.

# Mgombea ubunge CUF akemea ukabila

**Na Hamisi Nasri,** MASASI

WAKAZI wa Jimbo la Masasi Mjini, mkoani Mtwara wameshauriwa kuacha utamaduni wa kupenda kuchagua viongozi kwa kuangalia ukabila badala yake wachague kwa kuzingatia sifa bora za kiongozi ikiwamo kuthamini wananchi wake.

Kauli hiyo ilitolewa jana mjini Masasi na mgombea ubunge wa Jimbo la Masasi Mjini kwa Chama cha Wananchi (CUF), Hamza Machuma, alipokuwa akiwabutubia wananchi Wilaya ya Masasi kwenye mkutano wa kampeni za mgombea huyo pamoja na madiwani wa chama hicho, ambao ulifanyika katika viwanja vya Mti Mwiba Mjini Masasi.

Alisema Jimbo la Masasi Mjini kumekuwa na desturi kwa baadhi ya wananchi kuchagua viongozi kwa kuangalia tofauti za ukabila badala ya kuchagua kwa kuangalia sifa bora za uongozi.

Machuma alisema hakuna jambo baya kama kuchagua kiongozi kwa kuangalia ukabila wake kwani kuna uwezekano mkubwa wa kupata kiongozi ambaye hana uwezo wa kiutendaji, hivyo itakuwa ngumu kwa kiongozi huyo kusukuma maendeleo ya wananchi.

"Mimi wakati nafikirikia kugombea nafasi hii wapo walionifuata na kuniambia wewe ni Mmakonde, huwezi kupata ubunge kwani katika jimbo hili Wamakonde haweze kupata ubunge... sasa nisema mimi nitapata ubunge hata kama ni Mmakonde," alisema Machuma.

Alisema suala la ukabila lisiwagawe wananchi katika uchaguzi na kuwashawishi kuchagua kiongozi kwa kigezo hicho, na kwamba kiongozi bora hapatikani kwa ajili ya kabila lake.

Aidha, Machuma alisema iwapo wananchi hao wakimchagua kuwa mbunge, anaahidi kununua basi maalumu ambao litatumika kwa ajili ya kubeba wanafunzi kuwapeleka shuleni kila siku za masomo.

Alisema kipaumbele kingine ambacho atakitekeleza akiwa mbunge ni suala la kilimo hasa korosho, mbaazi, choroko na mahindi kuhakikisha yanakuwa na tija kwa wakulima tofauti na ilivyo hivi sasa.

Naye Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya CUF, Walindi Shaibu, alisema chama hicho kimejipanga kushinda majimbo yote 10 ya mkoa wa Mtwara kwa kuwa sera zake zina malengo chanya kwa wananchi wa mkoa huo.



Wakazi wa Jiji la Dar es Salaam, wakipita jirani na chemba ya majitaka, iliyoziba na kusababisha usumbufu na harufu mbaya kwa wakazi wa Mtaa wa Mlalakua, eneo la DDC- Mlimani, Kata ya Makongo, jana. **PICHA: FLORIDA RAYMOND-TUDARCo**

# Wahujumu miundombinu ya maji watangaziwa vita

**Na Tiganya Vincent,** UYUI

MKUU wa Mkoa wa Tabora, Dk. Philemon Sengati, ametangaza kiama kwa watu wanaohujumu miundombinu ya maji na kusababisha wananchi wenzao kukosa maji kwa sababu ya uharibifu uliofanyika.

Alitoa agizo hilo wakati wa ziara yake ya kukagua mradi wa majisafi na salama ya kisima katika Kata ya Loya wilayani Uyui, baada ya kusomewa taarifa na katibu wa jumuiya ya watumiaji maji ya kuwa kuna wizi wa mita na miunganishi katika Shule ya Sekondari Loya Bondeni.

Dk. Sengati aliagiza kukamatwa na kufikishwa katika vyombo vya sheria kwa watu wote watakaokutwa wakihujumu miundombinu ya miradi ya maji kwa kuiba vifaa na kusababisha wananchi kukosa maji.

Alisema serikali imetumia fedha nyingine katika kutekeleza miradi mbalimbali ikiwamo ya maji na vema jamii ikahakikisha inalindwa na haiharibiwa ili iweze kutumika kwa muda mrefu.

Alisema watakaokutwa wakiharibu au wakiiba vifaa ni lazima wakamatwe kwa makosa ya kuhujumu juhudi za serikali ya kuwasogezea wananchi maji karibu na makazi yao.

Aidha, aliwaagiza Wakala wa Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira (RUWASA) wilayani Uyui kuhakikisha wanatoa elimu kwa wananchi juu ya kulinda na kuitunza miradi ya maji ili iwe endelevu.

Dk. Sengati alisema ni lazima wananchi waelekezwe kuwa miradi hiyo ni mali yao na waweze kuzuia hujuma zozote endapo zitataka kutokea dhidi ya miradi yao.

Awali katibu wa jumuiya ya watumiaji maji wa Loya, Joseph Nduba, alisema hivi karibuni ulitokea uharibifu wa kuibwa kwa mita na viunganishio vya maji katika tangi la maji la Sekondari ya Loya Bonde na kusababisha upotevu wa maji katika eneo hilo.

Alisema walitoa taarifa katika kituo cha Polisi cha Loya na wanaendelea kuwatafuta waliofanya hujuma hiyo.

Nduba aliongeza kuwa katika kukabiliana na tatizo hilo, wameweka adhabu dhidi ya mtu yeyote watakayemkuta akiharibu chanzo cha maji na miundombinu yake.

## TANESCO yafagiliwa umeme wa Dodoma

**Na Friday Simbaya,** DODOMA

BODI ya Wakurugenzi wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), imeipongeza menejimenti ya shirika hilo kwa kasi kubwa ya utekelezaji na uendelezaji wa huduma za umeme wa uhakika, hivyo kuendana na kasi kubwa ya ukuaji wa Jiji la Dodoma.

Mwenyekiti wa Bodi ya TANESCO, Dk. Alexander Kyaruzi, alieleza kuwa kituo cha kupoza na kusambaza umeme cha Zuzu Dodoma, kina uwezo wa megawati 48, lakini kwa sasa zinatumika megawati 35 kulingana na matumizi yaliyopo.

Kwa mujibu wa Dk. Kyaruzi, ziada ni megawati 13 kwa Dodoma, lakini zitaongezwa tena megawati 250.

Aliongeza kuwa TANESCO inakamilisha upanuzi wa kituo cha Zuzu, upanuzi ambao utaongeza megawati hizo 250 za ziada, hivyo kuwezesha upatikanaji wa takribani megawati 300 kwa Jiji la Dodoma kuendana na kasi ya ukuaji wa jijini hilo.

Dk. Kyaruzi aliongeza kuwa kasi ya Jiji la Dodoma kupanuka kwa ujenzi wa makazi mapya, uwekezaji mpya, huduma za kijamii, ukuaji wa uwekezaji katika biashara pamoja na viwanda ni mkubwa, hivyo kufanya mahitaji ya umeme kuongezeka kwa kasi kila siku.

"Tumeridhishwa na kasi ya TANESCO baada ya kujionea kuwa wanakaribia kukamilisha upanuzi wa kituo cha Zuzu kwa kuongeza transfoma mbili kubwa zitakazoongeza megawati 250 za ziada. Ongezeko hilo litawezesha upatikanaji wa umeme mwingi na uwekezaji mkubwa jijini Dodoma," alisema Dk. Kyaruzi.

Dk. Kyaruzi aliongeza kuwa ndani ya Septemba upanuzi huo utakuwa umekamilika na umeme huo utakuwa tayari kwa matumizi kulingana na mahitaji yote jijini Dodoma.

Msimamizi wa mradi huo, Mhandisi Peter Kigadye, alieleza kuwa, TANESCO inatekeleza miradi mikubwa ya umeme kwa ustadi mkubwa ikitumia uzoefu ilioupata katika upanuzi na uendelezaji wa miundombinu katika majiji ya Dar es Salaam, Mwanza na Arusha.

"Tunatekeleza miradi hii ya upanuzi wa miundombinu ya umeme Dodoma kwa kutumia uzoefu mkubwa tulioupata katika majiji mengine tukizingatia ongezeko la makazi, biashara, viwanda pamoja na idadi ya watu," alisema Mhandisi Kigadye.

# Jamii yashauriwa kutembelea ofisi za mitaa

**Na Yasmine Protace**

JAMII imetakiwa kujenga utaratibu wa kushiriki katika mikutano inayoandaliwa na ofisi za serikali za mitaa, ili kujua miradi ambayo inaibuliwa katika maeneo yao.

Mbali na kujua miradi ambayo itaibuliwa katika maeneo yao, imeelezwa kuwa wanaweza kutumia mikutano hiyo kueleza kero ambazo zipo mitaani kwao ili ziweze kufanyiwa kazi.

Hayo yalisemwa na Ofisa Programu wa Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP Mtandao), Anna Sangai, katika semina za maendeleo ya jamii (GDSS) zinazotolewa na mtandao huo.

Alisema bajeti inatengwa kupitia mwongozo hadi ngazi za vijiji, mitaa na kata, lakini ushiriki wa wananchi katika kufuatilia na kuona bajeti iliyopo katika maeneo yao itatumika kufanya miradi gani.

"Inatakiwa wananchi wajenge utaratibu wa kushiriki mikutamo na kutembelea ofisi za serikali za mitaa waone kiasi cha fedha kilichotengwa na jinsi kitakavyotumika katika mradi huo," alisema Sangai.

Aliongeza kwa mujibu wa mwongozo wa kitabu cha bajeti, bajeti ya Tanzania inapofika Julai Mosi ndipo utekelezaji wa bajeti unapoanza, kwa maana ya fedha kuanza kutekeleza miradi.

Alisema jamii inatakiwa kufuatilia katika ofisi za serikali na kujua kama fedha zimefika ili zitumiwe na ziweze kuwekwa katika miradi.

Aliongeza kuwa Julai fedha zinapotolewa, jamii inatakiwa kujua kiasi kilichotolewa katika maeneo yao na kitatumika katika mradi gani.

"Kila mtu anatakiwa kujua bajeti iliyotolewa katika eneo lake na ajue itatumika kufanya shughuli ipi ya kimaendeleo," alisema.

Sangai alisema Agosti na Septemba ndipo yanapoanza maandalizi ya mwaka mwingine wa fedha.

Alisema bajeti inapoandaliwa kunakuwa na mwongozo ambao unaonyesha fedha zitakazotolewa zitakwenda kufanya kazi gani.




Meneja wa mwanasoka Mbwana Samatta, Alex Emmanuel, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam juzi, wakati wa uzinduzi wa huduma mpya ya Samapay inayomwezesha mteja kufanya manunuzi kwa njia ya mtandao. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Wakulima wauafiki mpango mbolea bure

**Na Mwandishi Wetu,** NZEGA

WAKULIMA mkoani Tabora wamepongeza mpango wa kampuni ya mbolea ya Yara Tanzania, wa kuwasaidia mbolea bure wakulima wadogo 83,000 nchini nzima kwani utachochea uzalishaji wa mazao ya chakula kwa familia nyingi.

Mpango huo unajulikana kama 'Action Africa' uliozinduliwa wiki iliyopita katika Wilaya ya Nzega mkoani Tabora, ambapo YARA imetenga tani 12,500 za mbolea ya YaraMila Cereal yenye thamani ya Sh. bilioni 16.5 inalenga kuinua kilimo cha mazao ya mahindi na mpunga nchini.

John Katara, mkazi wa Sikonge alisema mpango wa mbolea bure umekuja kipindi ambacho hata mfumo unaotumika wa kujisali ni mzuri na hautoi upendeleo kwa mtu yeyote kwani lazima mkulima aombe.

"Kinachotakiwa ni wakulima wadogo kuchangamkia fursa hii ili kujijengea uwezo na hatimaye kuwa na uhakika wa chakula. Uzalishaji wa mazao ya mpunga na mahindi utaongezeka," alisema Katara.

Edward Kasomambuto, mkulima wa mahindi wa Kaliua, amekaribisha mpango huo na kuomba elimu zaidi itolewe namna ya kujisali ili wakulima wengi weweze kunufaika zaidi na mpango huo.

"Ni matumaini yangu YARA inalengo nzuri la kumwinua mkulima mdogo kupitia mpango huu kwani njia bora ya kuwajengea uwezo wakulima wadogo ambao uwezo wao kumudu kununua pembejeo ni mdogo," alisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa YARA Tanzania, Winstone Odhiambo, aliwataka walikuma nchini kujitokeza na kujisajili na kunufaika na mpango huo wa kugawa mbolea bure.

Alisema kampuni yake imejielekeza zaidi kuwainua wakulima wadogo hapa nchini sambamba na kuhakikisha kuwa dhamira ya serikali ya Rais John Magufuli ya kuleta mageuzi katika sekta ya kilimo inafikiwa.

"Tumejipanga pia kuhakikisha mbolea hii tani 12,500 chini ya mpango wa 'Action Africa' inawafikia wakulima kwa wakati. Zoezi la ugawaji wa mbolea litafanywa kwa uwazi na kuwaomba wakulima kijisajili.

Akizindua mpango huo, Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Dk. Philemon Sengati, aliwataka wakulima kutumia vizuri fursa hiyo.

Alisema kampuni ya YARA imekuwa mdau muhimu katika maendeleo ya sekta ya kilimo katika mkoa wake na kwamba atashirikiana nayo kuhakikisha mkulima mdogo na wakati ananufaika na kilimo.

Sherehe ya uzinduzi ilihudhuriwa na Naibu Waziri Kilimo, Hussein Bashe ambaye alisema serikali itaendelea kuweka mazingira mazuri ya kuvutia uwekezaji katika sekta ya kilimo.

"Kama serikali tumeshachukua hatua mbalimbali kuhakikisha kuwa sekta ya kilimo nchini inaanza kukopesheka kwa gharama nafuu kutoka asilimia 22 mpaka asilimia 13," alisema.

# Mgombea ACT ajinadi na kero za afya, viwanja

**Na Said Hamdani,** LINDI

MGOMBEA udiwani Kata ya Rasbura, Jimbo la Lindi Mjini kupitia Chama cha ACT-Wazalendo, Abbasi Said Nng'wachi, amewaomba wakazi wa kata hiyo kumchagua ili kutatua kero mbalimbali, zikiwamo afya, miundombinu na viwanja.

Alidai kuwa aliyekuwa diwani kupitia CCM, Abdallah Chikwei, alishindwa kuzitatua kero hizo kwa miaka 25.

Nng'wachi akiomba ridhaa kwa wananchi waliojitokeza kumsikiliza kwenye mkutano wa kampeni, alisema kilichomsukuma kuwania nafasi hiyo ni kutokana na wananchi kuendelea kuteseka kutokana na kero hizo kwa muda mrefu.

Alisema wananchi wameshiriki kuchanga fedha na nguvu zao na kwa ajili ya miradi mbalimbali, lakini umekosekana usimamizi wa diwani.


"Ninachowaomba ndugu zangu, wazee wangu na vijana wenzangu nichagueni ili nishirikiane nanyi katika kuondoa changamoto zilizopo," alisema Nng'wachi.

Mgombea huyo ametaja changamoto zingine atakazozisimamia na kuzitekeleza akipewa ridhaa ya kuiongoza kata hiyo ni kuhakikisha miundombinu ya barabara inaboreka na upatikanaji wa viwanja vya makazi, ambavyo kazi ya upimaji wake imeshafanyika miaka 37 iliyopita.

Kwa upande wake mgombea ubunge Jimbo la Lindi Mjini, Ishaka Rashidi Rashidi Mchinjita, aliwaomba wananchi kutorudia makosa kwa kuwachagua wagombea wa CCM kwa kile alichokieleza wamekuwa hodari wa kuahdi mambo bila ya utekelezaji.

Mchinjita amesema mara nyingi CCM imekuwa ikiahidi mambo mbalimbali kwa wananchi wa Mkoa wa Lindi, ukiwamo ujenzi wa kinu cha kuchakata gesi asilia eneo la Likong'o, Kata ya Mbanja, lakini hakuna kinachoendelea, badala yake imekuwa ikitoa ahadi zisizokwisha.

Pia, aliwaomba wana-Lindi na maeneo mengine kutompigia kura mgombea yeyote wa CCM badala yake wageukie upande wa upinzani.




Ukurasa 13

Tukienzi Kiswahili basi kama tumeamua



Ukurasa 12

**Uwekezaji UTT unavyookoa kipindi cha ukata**

BUFE
IJUMAA SEPTEMBA 11, 2020
Nipashe
BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA



# Wasomi UDSM kuanza kupikwa kiujasiriamali

## •Ni ili kuwaondolea kiu ya kuajiriwa
## •2021 wahitimu 250 kuonyesha matunda

**Na Sabato Kasika**

BAADA ya wahitimu wa vyuo vikuu kumaliza shule bila stadi za ubunifu, utafutaji na ujasiriamali na kujikuta wakiwa waathirika wa kusaga lami kutafuta kazi, adha hiyo sasa inaelekea ukingoni.

Hii ni kutokana na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na wadau wa elimu kuanzisha programu ya kuwapatia nyenzo za ubunifu na kuwajengea kiu ya kujiajiri badala ya kusubiri kuajiriwa.

Chuo hicho kinafanya jitihada ili wasomi watakaohitimu mwaka 2021, wawe wameiva na kuwa tayari kujiajiri na kuachana na mazoea ya kutegemea ajira rasmi kutoka sekta ya umma na binafsi.

Profesa Bernadeta Killian, Naibu Makamu Mkuu wa chuo hicho (Utafiti), anaelezea mkakati huo kuwa unaendana na ajenda ya mabadiliko ya uchumi wa Tanzania kwa kufanya uwekezaji ili kuwapa maarifa zaidi.

Anasema, hatua hiyo itawezesha taasisi za elimu na kampuni za kibiashara kushirikiana kuwapa uratibu na utekelezaji wa mpango wa kutoa ujuzi unaotakiwa katika karne ya 21.

Anasema, hayo mwishoni mwa wiki iliyopita wakati wa kuwekeana makubaliano ya miaka mitano kati ya chuo hicho na Kampuni ya Empower Limited ya jijini Dar es Salaam ya kusaidiana kutoa elimu hiyo.

"Lengo la kufanya hivyo, ni kutaka wanafunzi wanapohitimu, wasiwaze kuajiriwa zaidi bali watumie ujuzi huo kujiajiri ama kufanya shughuli mbalimbali za kuwaingizia kipato," Profesa Killian Anasema.



Mkurugenzi Mtendaji wa Empower Limited, Miranda Naiman (kulia), katika uzinduzi wa makubaliano ya mafunzo ya ujasiriamali na ubunifu. Katikati ni Naibu Makamu Mkuu wa chuo (Utafiti), Prof. Bernadeta Killian na Mkurugenzi Ubunifu na Ujasiriamali, Dk. Ambrose Itika. **PICHA: SABATO KASIKA**

**MATARAJIO KIMAFUNZO**

Profesa Killian anasema, awamu ya kwanza ya mafunzo ya programu hiyo itajumuisha wanafunzi 250 kutoka fani tofauti za kitaaluma kwa mwaka mzima, kufanikisha mkakati wa kuwanoa walengwa ili wapate ujuzi unaotakiwa.

"Chuo Kikuu kinafurahi kushirikiana na Empower kuleta mabadiliko chanya yanayowezesha kuwapatia ujuzi wa karne ya 21 wanafunzi 250 kila mwaka, sambamba na maarifa ya kusimamia vipaji vyao," anasema.

Profesa Killian anasema, hatua hiyo pia itasaidia kuwawezesha wanafunzi kuchangamana na wateja wa kampuni za kibiashara, hivyo ninatoa wito kwa kampuni hizo kuunga mkono programu hiyo iitwayo GenEm.

"Ushirikiano huo unaendana na ajenda ya mabadiliko ya uchumi wa nchi kwa kufanya uwekezaji ili kuwapa wahitimu maarifa, ambao utawezesha taasisi za elimu, kampuni za kibiashara kushirikiana kuwapa uratibu mzuri na utekelezaji wa mpango wa kutoa ujuzi unaotakiwa katika karne ya 21," anasema.

Anafafanua kuwa kila mwaka wanafunzi wa fani mbalimbali wanahitimu katika chuo hicho, hivyo suala la kutoa elimu ya ujasiriamali na ubunifu ni muhimu ili wanapohitimu wawe na cha kufanya badala kusubiri ajira.

KUANZA MAFUNZO

Mkurugenzi Mtendaji ambaye pia ni muasisi wa kampuni ya Empower Limited, Miranda Naiman, anasema, mafunzo hayo ya programu ya GenEm, yataanza Novemba mwaka huu.

"Yataendeshwa kwa njia shirikishi na kwa vitendo zaidi huku wanafunzi wakishiriki katika semina za kubadilishana mawazo na mafunzo kutoka kwa wataalam," anasema Miranda.

Anaeleza kuwa GenEm itawapa wanafunzi hao maarifa zaidi ya taaluma zao na kuunganishwa katika fursa za ajira mara wanapohitimu na kampuni zinaweza kufaidika na hao wenye ujuzi mkubwa na vipaji.

Anasema, watatoa elimu hiyo kwa kuzingatia mipango ya kitaaluma ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kwa kuwapa wanafunzi watakaofanikiwa kupitia programu hiyo ujuzi unaotakiwa kwa sasa.

"Vilevile, wanafunzi watapata mada kutoka kwa viongozi wa tasnia mbalimbali na mwisho washiriki watafanya miradi kwa vitendo kuhusiana na mafunzo waliopata," anasema.

Miranda anasema, UDSM na Empower, wanawakaribisha wadau kushiriki katika GenEm, zikiwamo sekta binafsi, watunga sera na washirika wahisani ili kufanikisha jitihada za kutoa na kuendeleza juzi.

"Ujuzi huo ni kupitia mpango wa ubia kati ya taasisi za umma na binafsi (PPP). Programu hii ni ya kwanza kuanzishwa nchini na kuendeshwa kwa njia ya kipekee, huku maudhui ya mafunzo yanayotolewa yanasimamia na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Miranda anasema, lengo ni kuhakikisha mafunzo yanakidhi viwango vinavyotakiwa kwa kila tasnia, na kwamba Empower inayoyatajarisha inahakikisha yanathibitishwa na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

"GenEm inawezeshwa na Idara ya Uwezeshaji vijana

ENDELEA UK.14

BIASHARA

# Uwekezaji UTT unavyookoa kipindi cha ukata

## •Hulipa ada, bima na kukuwezesha kujikimu



Ofisa wa UTT -AMIS Martha Mashiku akitoa maelezo kwa Waziri wa Uwekezaji Angela Kairuki, namna uwekezaji unavyonufaisha wanachama.**PICHA : UTT-AMIS.**

**Na Frank Monyo**

KATIKA kufanikisha maendeleo ya watu na taifa, mbinu mojawapo inayotumika ni uwekezaji unaonyanyua uchumi wa mtu mmoja mmoja na wa taifa kwa wakati mmoja.

Ndiyo maana zama hizi kumekuwa na mwamko wa Watanzania kujikita katika uwekezaji wa aina mbalimbali hasa katika kampuni zinazojihusisha na miradi inayoinua uchumi wao na wa taifa pia.

Katika jitihada hizo Kampuni ya Unit Trust of Tanzania UTT AMIS (UTT-AMIS) iliyo chini ya Wizara ya Fedha na Mipango, imewapa wananchi kipaumbele na ina mchango kwa Watanzania na taasisi za kimataifa kuchochea maendeleo ya uchumi katika jamii na taifa kwa ujumla.

UTT AMIS inayosimamiwa na Wizara ya Fedha kwa miaka 10 sasa, imekuwa ikitoa fursa kwa Watanzania wenye vipato vya aina zote na nyadhifa tofauti kuwekeza kwa manufaa yao, watoto na taifa kwa ujumla.

Ofisa Mwandamizi wa Idara ya Masoko na Mahusiano wa UTT AMIS, Rahim Mwanga, anasema taasisi hiyo ina jukumu la kuanzisha na kuendesha mifuko ya uwekezaji wa pamoja kwa mujibu wa sheria ya masoko ya mitaji na dhamana ya mwaka 1994 pamoja na marekebisho yake na kanuni zake za 1997.

### MALENGO YA KUANZISHWA

Mwanga anabainisha kuwa, serikali ilikuwa na lengo la kuleta wigo mpana kwa wananchi kuwawezesha kuweka akiba na kuwekeza akiba kupitia masoko ya fedha na mitaji ili kushiriki kikamilifu katika kumiliki uchumi wa nchi kutokana na mabadiliko ya sera za kiuchumi katika nyakati hizo.

Anaendelea kusema kuwa serikali ilitaka kuleta ushiriki mkubwa wa wananchi kwenye uchumi kwani kulikuwa na sera ya ubinafsishaji wa kampani na mashirika ya uma, kukawa na changamoto kubwa kwa Watanzania.

"Changamoto hiyo ilikuwaje, baada ya hatua hiyo na kufunguka kwa uchumi wa soko? Mtanzania anapata manufaa gani na uwepo wa masoko ya fedha na mitaji?" anasema na kuongeza;

"Wakati wa sera ya ubinafsishaji na matokeo yake, ndipo ilianzisha Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA) na Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE), iliyofanya wananchi wenye vipato vya chini na vya kati kunufaika na masoko hayo," Anaongeza kuwa kulitakiwa kuwapo na daraja ambalo lingewawezesha kushiriki kikamilifu na kwa gharama ndogo zaidi, hivyo kukaanzishwa Unit Trust of Tanzania ili kuja na mfumo ambao unawezesha wananchi wote wa vipato vya chini na vya kati kuwekeza mitaji pamoja na kushiriki kwa urahisi kwenye masoko ya fedha na ya mitaji.

"UTT ilivyoanzishwa ikaja na mfumo ambao utawezesha watu wa aina zote kushiriki tena kunufaika. Ikianzisha mfumo wa uwekezaji kupitia mifuko ya uwekezaji wa pamoja," anasema Mwanga.

### MIFUKO INAFANYAJE KAZI

Mwanga anasema kuwa UTT AMIS inapata leseni kutoka Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na dhamana inayowawezesha kukusanya amana kutoka kwa wawekezaji na kuziwekeza.

"Tukishapata fedha hizo tunaenda kuwekeza katika mfuko husika kulingana na waraka wa toleo la mfuko tuliyonayo inayowekeza katika sehemu kubwa mbili ambazo ni masoko ya fedha na masoko ya mitaji. Faida inayopatikana inarejeshwa na kugawanywa kwa wawekezaji na sehemu ya uwekezaji wao katika mfuko ndiyo inafahamika kama kipande," anasema Mwanga.

### MASOKO YA MITAJI NI YAPI?

Ofisa huyo anafafanua kuwa masoko ya mitaji ni masoko ya fedha yenye kuhusisha dhamana za uwekezaji za muda wa zaidi ya mwaka mmoja.

"Mfano kuna kuwekeza kwenye hisa ambazo zimeorodheshwa na Soko la Hisa Dar es Salaam (DSE) pia kuna kuwekeza kwenye hati fungani za muda mrefu na za serikali au zile fungani ambapo hapa mwekezaji anaikopesha serikali kwa muda mrefu na baadaye inamlipa kwa mujibu wa makubaliano," amesema Mwanga. Anaeleza kuwa masoko ya fedha yanahusisha dhamana za uwekezaji za muda mfupi ambazo hupevuka chini ya mwaka mmoja. Mfano dhamana za serikali za muda mfupi na akaunti za uwekezaji za muda maalumu katika benki za kibiashara.

### FAIDA UWEKEZAJI PAMOJA

"Faida katika uwekezaji huu wa pamoja ni mwekezaji kuwa na nafasi ya kupata faida shindani ukilinganisha na bidhaa za uwekezaji wa namna hiyo katika soko. Hatari za uwekezaji zikipunguzwa kwa kufanya uwekezaji mseto," anasema Mwanga.

Anaongeza:"Pia mifuko ya uwekezaji inawezesha wawekezaji wadogo kupata fursa za kuwekeza kwenye masoko ya fedha na mitaji kwa viwango vidogo vya fedha tena mara kwa mara.Kuna fursa ya kuwekeza kwenye dhamana ambazo katika hali fulani mwekezaji mmoja moja inakuwa ni ngumu au ghali kuweza kupata dhamana hizo,"

Anasema mwanachama kwa kuwekeza kwenye mifuko ya pamoja anapata utaalamu wa Meneja Mwendeshaji wa UTT AMIS. Vilevile ni rahisi kwa mwekezaji kufuatilia mwenendo wa amana zake kupitia thamani ya kipande cha mfuko husika ambapo hutolewa kila siku ya kazi.

Mwanga anasema kuwa anapohitaji kuuza vipande vyake, Meneja wa Mfuko huvinunua hivyo kumwakikishia mwekezaji uhakika wa kuweza kupata fedha zake kwa wakati sawa na vigezo vya mfuko husika, kawaida ni ndani ya siku tatu hadi 10 za kazi.

### NAMNA MIFUKO ILIVYOANZA

Mwanga anafafanua kuwa, mfuko wa awali na maarufu ulianza mwaka 2005 unaofahamika kama mfuko wa umoja ambapo kwa wakati huo ili kuleta ushiriki kikamilifu, serikali ilielekeza vipande viuzwe kwa bei ya punguzo ambayo ni Sh. 70 badala ya Sh. 100 huku Sh. 30 ikibebwa na serikali, yote ikiwa na maana ya kuleta ushiriki mkubwa pamoja na watu kuelewa vyema mfumo huo.

"Hivyo, tulianza mkakati huo tukiwa na mfuko huo wa umoja pekee, lakini hasa kwenye dhana ya kuwezesha wananchi kwamba mifuko hiyo ya uwekezaji wa pamoja inamwezesha mwananchi mwenye kipato kidogo, kikubwa na cha kati wote kushiriki kwenye kuwekeza na kunufaika na uchumi hasa kwenye sekta ya masoko ya fedha na mitaji kwa kuwekeza kidogo kidogo.

"Mfuko wa umoja ulipoanza kiwango cha chini cha kuwekeza ilikuwa vipande 10 ambapo kwa wakati huo ilikuwa Sh. 70 na mwanachama angetakiwa kununua kwa Sh. 3,500 ili watu wengi waweze kushiriki.

"Hata hivyo kwasasa mfuko umekuwa na wawekezaji wengine wameshanufaika na sasa thamani ya kipande ni Sh 638 ikiwa na maana kwamba kwa aliyewekeza tangu 2005 na fedha yake hakutoa hadi sasa 2020 fedha yake imekuwa zaidi ya mara tisa mfano kama aliweka Sh. 1,000,000 amefikisha 9,000,000 anasema Mwanga.

Aidha, anafafanua zaidi kuwa, dhana kubwa ilikuwa ni kuwawezesha wananchi kuwekeza akiba na kukuza mitaji ili waweze kuwekeza zaidi katika sekta nyingine za kiuchumi.

"Kwa sasa UTT AMIS inaendesha mifuko sita ambayo ni Umoja wa wazi wenye uwiano sawa wa uwekezaji unaoufanya kuwa mfuko bora wenye hatari za uwekezaji wa kiwango cha kati.

### MFUKO WA UMOJA

Mwanga anasema Mfuko wa Umoja ambao unawekeza kiwango kisichozidi asilimia 50 ya fedha zake kwenye hisa zilizoorodheshwa kwenye Soko la Hisa la Dar es Salaam na kiasi kisichopungua asilimia 50 huwekezwa kwenye masoko mengine ya fedha na mitaji yenye sifa tofauti.

Anaeleza kuwa hivi sasa kiwango cha chini cha kuanza kuwekeza kwenye mfuko huu ni Sh. 6,500.

### MFUKO WA WEKEZA

"Mfuko wa Wekeza Maisha ni uwekezaji ulioambatanishwa na faida za bima. Ni mpango wa uwekezaji wa muda wa miaka 10. Mwekezaji anaweka lengo la kiasi anachotaka kuwekeza katika muda huo wa miaka hiyo. Kiwango cha chini ni Sh. 1,000,000. Anaweza kuwekeza kwa mkupuo au awamu," anaongeza.

"Endapo atachakua kuwekeza kiasi hicho kila mwezi atahitajika kuwekeza Sh. 8,340 ili kukamilisha mpango wake wa uwekezaji. Zaidi ya asilimia 99 ya fedha za mwekezaji huwekezwa na chini ya asilimia moja hutumika kugharimia bima. Bima zitolewazo na mfuko ni ya maisha, ulemavu wa kudumu na ajali,"

### MFUKO WA WATOTO

"Mfuko wa watoto wenye lengo la kumpatia fursa mzazi kuanza kuweza mapema kwa ajili ya elimu ya sekondari hadi chuo kikuu ya mwanaye. Kiwango cha chini cha kuanza kuwekeza ni Sh. 10,000 na cha chini cha nyongeza ni 5,000." anaeleza Mwanga

### MFUKO WA KUJIKIMU


Mwanga anasema kuwa Mfuko wa Kujikimu una lengo la kutoa gawio la mara kwa mara huku ukilenga kukuza mtaji kwa wawekezaji wa muda mrefu.Mfuko hutoa gawio kila baada ya miezi mitatu au baada ya mwaka. "Ili uweze kupata gawio kila baada ya miezi mitatu kiwango cha chini cha kuchangia ni Sh. 2, 000,000 na kupata gawio kila mwaka kiwango cha chini 1, 000,000.Hakuna ukomo wa kiwango cha juu kuwekeza," anasema Mwanga.

### MFUKO WA UKWASI

"Mfuko wa Ukwasi ni mpango ulio wazi unaotoa njia nyingine ya uwekezaji kwa wanachama wanaotaka kuweka fedha zao kwa kipindi cha muda mfupi na katika kiwango kilichopo kwenye ushindani. Hatari au athari kidogo katika uwekezaji na ukwasi wa hali ya juu ndilo dhumuni hasa la mfuko huu. Kiwango cha chini cha kuwekeza ni Sh. 100,000 na kiwango cha chini cha nyongeza ni 10,000. Hakuna kikomo katika kiwango cha juu cha kuwekeza," anasema Mwanga

TAFAKURI YA MLALAHOI

# Tukienzi Kiswahili basi kama tumeamua






**NA JOSEPH KULANGWA**

"NI aibu sana kwa Tanzania kama kitovu cha Kiswahili, biashara zake kuwa na maneno ya Kiingereza." Ni kauli ya Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Harrison Mwakyembe, kwa Baraza la Kiswahili Tanzania (BAKITA) hivi karibuni.

Alilitaka baraza hilo kutumia kanuni za Sheria ya Mwaka 1967 iliyoboreshwa mwaka 2019 inayotoa adhabu kwa wanaopotosha lugha ya Kiswahili.

Kauli hii inapaswa kuungwa mkono na kila Mtanzania anayeenzi Kiswahili, hususan wakati huu ambao nchi imedhamiria kuhakikisha lugha hiyo inatumika na kuendelea kukua hata nje ya mipaka.

Ni jambo la kusikitisha, kwamba Tanzania ambako ndiko chimbuko la Kiswahili Afrika, bado lugha hii haipewi kipaumbele na baadhi ya watumiaji hata kubembelezwa kuitumia, kana kwamba tumeiazima kutoka Taifa lingine, huku majirani wakitamani kuitumia hata kuliko sisi.

Watanzania kwa bahati mbaya sana,tumejikuta malimbukeni wa lugha za kigeni na kusahau utamaduni wetu, ambao ndio msingi wa matumizi ya lugha hii ya Kiswahili. Tumeingia kwenye mkondo wa kuamini kwamba msomi ni anayezungumza Kiingereza au lugha nyingine ya kigeni.

Mtanzania akilewa atazungumza Kiingereza ili aonekane ni wa kisasa, mwanamuziki akiimba wimbo wa Kiingereza, ataonekana ni wa kileo zaidi.

Mbunge akichangia hoja bungeni akachanganya na Kiingereza, ndivyo atajisikia ameitendea haki hoja! Ni mambo ya kushangaza tu.

Lakini, hata katika taaluma, wapo wanaoamini kuwa endapo lugha ya kufundishia itakuwa Kiswahili, basi wafundishwao watakuwa hawajaipokea barabara elimu wanayopewa, kwa kuwa elimu ya kisasa chimbuko lake ni Ulaya.

Licha ya Dk. Mwakyembe kuchelewa kusisitiza hilo, bado fursa ipo ya kufanya mabadiliko makubwa katika matumizi ya lugha na kufanya bidhaa ze tuna hata taasisi tulizo nazo, kuacha kutumia maneno ya Kiingereza, kuanzia majumbani hadi serikalini.

Hivi kama kweli tunataka Kiswahili tukitumie kikamilifu na kukienzi, kwa nini leo taasisi ya serikali iitwe… Corporation na si Shirika…?

Ndiyo, tuna Baraza la Taifa la Kiswahili (BAKITA), tuna Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA) safi kabisa…

Haya mambo ni mengi, na ndiyo sababu kuna Yanga SC (Sports Club) na si Klabu ya Michezo ya Yanga (KM Yanga) au Simba SC ikawa KM Simba? Tunaenzi vipi Kiswahili na uzungu huu?

Kongole iende kwa magazeti ya Kiswahili, yanakienzi Kiswahili na ya Kiingereza hali kadhalika kwa lugha hiyo, lakini kwingineko huku tunapaswa kubadilika ili kuenzi lugha yetu mama, si kwa majina ya watu tu, bali pia kwa majina ya baa, kampuni za mabasi na kadhalika.

Inapendeza pia hata kwenye magari ya serikali ambayo yanatumiwa na wazito na hata manaibu wao, vibao vya namba vigetambuliwa kwa majina ya Kiswahili

Huenda tunaona aibu kutumia majina yetu ya Kiswahili na hiyo inafika mpaka hata kwa majina yetu binadamu. Mtu anabadili ili mradi jina lionekane la kizungu. Ulimbukeni uliopitiliza!

Kwani kulikuwa na haja ya kuwa na majina makubwa kwa kizunguzungu katika katika majengo ya kitaifa? Mtasema baadhi yanatumika kimataifa, kwa kuwa wageni wa mataifa mbalimbali, nitauliza kwani tumewajengea wao au Watanzania Waswahili? Tutumie lugha yetu wageni wajao wajifunze. Alamsiki!

**•Simu +255 713 410008 na baruapepe: jkulangwa@yahoo.com**

BIASHARA

# Mipakani waziambia benki riba ni mwiba wa uwekezaji

**Na Yasmine Protace**

UWEZESHAJI kimitaji ni njia inayomkomboa mjasiriamali anayetamani kuinukia kiuchumi lakini anakwamishwa na fedha, vitendekazi, ardhi na bidhaa za kufanyia biashara.

Mitaji iwe ya pesa, mifugo, mashine au ardhi na miundombinu ndiyo inayowawezesha watu kuanza biashara ya bidhaa na huduma au uzalishaji kulingana na kile wanachokitaka.

Kama walivyo wajasiriamali wengine, wanawake wanaofanyabiashara mipakani wanalitaja suala la mitaji kuwa ni changamoto inayowakumba.

Aidha, wanasema kuwa hata wanapopata mitaji hiyo ambayo ni mikopo ya benki , wanachajiwa riba kubwa.

Wanayasema hayo kwenye mafunzo yanayotolewa na TGNP Mtandao kuwainua kiuchumi. Pamoja na uwezeshwaji huo kimafunzo,baadhi ya wafanyabiashara hao wa mipakani wanaziomba taasisi za fedha kuwawezesha mikopo yenye riba nafuu ambayo itawasaidia hao kurejesha pesa kwa haraka.

Wanasema mbali na riba kubwa, pia baadhi ya benki kutowapa mikopo au mitaji hiyo kwa wakati ni miongoni mwa mambo yanayowakwamisha kiuwekezaji.

Mwenyekiti wa Wafanyabiashara wa Mipakani Beatrice Yohana, katika mafunzo ya kuwajengea uwezo wa kufanya biashara na kuinuka kiuchumia kupitia taasisi za kifedha, anasema licha ya changamoto wanafanya biashara Kenya, Uganda, Rwanda na Burundi.

Anasema katika kuzikuza biashara zao taasisi za kifedha zinatakiwa kuwapa mikopo yenye riba nafuu kwani wapo wanawake wanaotamani kufanya biashara ili wajiinue kiuchumi, lakini wanakutana na changamoto za kupata pesa kwa marejesho ya riba ndogo.

"Benki zinatakiwa kufikiria namna bora zaidi ya kuwawezesha kiuchumi wafanyabiashara wanawake wenye mitaji midogo na si kuwachukulia kama walio na mitaji mikubwa,"anasema Beatrice.

Anazitaja changamoto nyingine ambazo wanakumbana nazo katika biashara zao mipakani kuwa ni baadhi ya wafanyabiashara kutojua sheria hasa zinazohusiana na mikopo .

Faith Swai, Ofisa Mikopo wa Equity Bank, akizungumza na wafanyabiashara hao, anasema wamepatiwa elimu ya fedha kwenye utunzaji fedha ili waweze kuinuka kiuchumi.



Kinamama wajasiriamali wanaofanya biashara mipakani mwa Kenya, Uganda na Tanzania baada ya kuhitimu mafunzo **.PICHA: JASMINE PROTACE.**

Anasema mbali na elimu ya kutunza fedha pia wamepatiwa mbinu za kunufaika na fursa zilizopo na zinazotolewa na benki.

Anasema wamekuwa wakitoa mafunzo kwa kina mama wafanyabiashara mipakani kutokana na benki yao kuwa mipakani.

Kwa mujibu wa Swai, wafanyabiashara wakinamama wa mipakani walikuwa baadhi yao hajui kama kuna fursa katika mabenki ambazo zina mchango mkubwa katika kukuua biashara zao.

Ofisa huyo anasema fursa hizo zinawasaidia kujiongezea vipato katika biashara , kukua kwa mitaji ikiwamo kujulikana kwa wafanyabiashara wakubwa na kujitangaza kupitia bidhaa wanazozalisha.

Benki yao inatambua mchango wanaotoa akina mama na wamekuwa wakiwapatia mikopo yenye riba ndogo na elimu ya biashara, anasema Swai.

Anaongeza kuwa benki yao ina kanuni ya kuwawezesha kukuza biashara na kuwaunganisha na wafanyabiashara wenzao waliopo katika nchi jirani.

Anasema wafanyabiashara hao wamewezeshwa kufanya biashara kwa urahisi na usalama zaidi kwa kutosafiri na pesa zao jambo ambalo ni hatari na wakati mwingine linaweza kusababisha kupotea maisha na mali au kujeruhiwa na wahalifu.

Anaongeza kuwa changamoto ambayo wameiona kwa wafanyabiashara hao ni kutokuwa na elimu ya biashara ambalo ni tatizo pia hawajui kama kuna fursa kwenye benki wanazoweza kunufaika nazo.

Anasema benki hiyo inawasaidia wanawake kwa kuwapatia mikopo yenye riba nafuu na ndogo, pia ina utaratibu wa kuwaunganisha wanawake katika vikundi na kuwapatia elimu ya fedha.

Amina Sabani ni mmoja wa wafanyabiashara wa mipakani aliyenufaika na mafunzo waliyoyapata akisema yatawasaidia kuongeza ushindani katika biashara zao hasa kwenye maeneo ya mipakani.

Anasema changamoto walizokuwa wakizipata baadhi ya wafanyabiashara hao ni kukaa na pesa nyingi bila kuwa na akaunti na hilo liliwasababishia upotevu.

Anasema mafunzo hayo yamewaimarisha katika kuboredha biashara zao ikiwa ni pamoja na kupata mikopo yenye riba nafuu na kuelewa mbinu za utafutaji.

" Ili tupige hatua inatakiwa elimu ya biashara itolewe. Na sasa tumepata utaalamu na ujuzi tunaambiwa mikopo ipo na tena yenye riba ndogo ni sisi tuchukue hatua,"anasema mjasiriamali huyo.

Anaongeza kuwa wamefurahi kuona benki ya Equity inatoa huduma katika maeneo ya mipakani, na sasa hawatatembea ovyo na pesa kwani wanaziweka katika benki na itakuwa ni usalama zaidi kwao.

Hamida Jamal, mmoja wa wafanyabiashara wa mipakani anasema mafunzo ni moja ya mafanikio katika biashara na kwamba bila ujuzi hakuna mafanikio.

"Kutokana na kupata mafunzo mara kwa mara kutoka TGNP Mtandao, wameboresha bidhaa zao kwa kiwango kikubwa hata katika upande wa vifungashio, viwango bora na utafutaji masoko".

**BIDHAA MIPAKANI**

Hamida anataja bidhaa ambazo wanauza mipakani kuwa ni unga wa lishe, sabuni za maji, batiki, viatu vya asili, mafuta ya kupikia, urembo na vitu vingine vinavyozalishwa Tanzania.

Anasema kutokana na kuzingatia mafunzo ya biashara wameandaa bidhaa zenye ubora zaidi, kupata wanunuzi zaidi kutoka ndani ya nchi na nje ya nchi hasa wateja wa nchi jirani.

Gema Akilimali kutoka TGNP Mtandao anawataka wafanyabiashara hao kuyazingatia mafunzo waliyoyapata ili yawasaidie kuboresha bidhaa zao na kuinuka kiuchumi.

Anawakumbusha kuwa wameelimishwa kuhusu utunzaji fedha,ukopaji mikopo,fursa zilizopo katika benki na mbinu za utafutaji na kuwashauri kuwafikishia wenzao utaalamu huo.

Suzy Masala, mwezeshaji wananchi kiuchumi kutoka Baraza la Kitaifa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NECC), anasema baraza linatekeleza uwezeshaji wanawake kwa kuwafundisha program zote za uwezeshaji na masuala ya jinsia.

Anasema baraza hilo ni chombo cha juu cha uongozi kwa ajili ya kusimamia utekelezaji wa Sera ya Taifa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ambao unafanywa na sekta zote.

Akizungumzia ushiriki wa Watanzania katika uwekezaji, anasema NEEC inaratibu na kuongoza utekelezaji wa mpango wa baraza hilo kwa mkakati wa miaka 10 na kusisitiza kuwa

ujasiriamali ni nguzo ya Sera ya Taifa ya Uwezeshaji

ambayo inalenga kuinua viwango vya ujuzi na uzoefu .

Anasema baraza limeshirikiana na wadau kutengeneza mkakati wa ujasiriamali, mwongozo wa kufundisha wajasiriamali, kutambua watoa huduma wa maendeleo ya biashara ya kiwango kidogo na cha kati.

Akizungumzia ushiriki wa vikundi vya ushirika anasema kuwa, Tanzania ina jumla ya vyama vya ushirika 10,620 kwenye maeneo mbalimbali vyenye wanachama takribani 2,500,000 vya kijamii na vya kiuchumi ni takribani 200,000 na wanachama wake ni 4,500,000 ambao NEEC inawahudumia.

# WASOMI UDSM KUANZA KUPIKWA KIUJASIRIAMALI

**INATOKA UK.11**

kwa kushirikiana na Kitengo cha Ubunifu na Ujasiriamali cha Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDIEC), ambacho kimejipanga kuhakikisha kinaongoza barani Afrika kwa kutoa mafunzo ya ujasiriamali na ubunifu," anasema.

Mkurugenzi Ubunifu na Ujasiriamali wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Dk. Ambrose Itika, anasema chuo hicho kilianzisha kitengo cha Ubunifu na Ujasiriamali mwaka 2016.

"Lengo ni kusimamia na kuendeleza ubunifu na ujasiriamali, ili wahitimu wawe pia na mawazo ya kujiajiri badala ya kutegemea kuajiriwa tu, na tunafurahi kupata watu hawa wanaotuunga mkono," Dokta Itika anasema kwa kushirikiana na kampuni hiyo, wamepania kupunguza idadi ya wahitimu wanaozunguka na vyeti kutafuta, badala yake watumie elimu ya ubunifu na ujasiriamali kujiajiri.

"Siyo kwamba mhitimu asiajiriwe, bali hata anapoajiriwa, basi utumie ubunifu kufanikisha kazi atakayoifanya, hivyo ninaamini kwamba wanafunzi 250 ya kwanza watakapoanza programu Novemba, watatoka wakiwa wameiva tayari kuajiriwa ama kujiajiri," anasema.

**AJIRA NCHINI**

Takwimu za serikali zinaonyesha kuwa tatizo la ajira bado ni kubwa, hivyo njia pekee ya kulipunguza ni kushirikiana na sekta binafsi katika kuwajengea uwezo vijana kuzalisha ajira.

Januari mwaka huu, Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Ajira na Walemavu, Anthony Mavunde, anasema hayo katika shindano la wajasiriamali wana vyuo la Global Student Entrepreneur Award (GSEA).

Anasema, serikali inafarijika kuona taasisi zinajitokeza kuwasaidia kuwajengea uwezo vijana, kuweza kujiajiri na kutoa ajira kwa wengine, itashirikiana nazo kuhakikisha wanatimiza lengo hilo.

"Tutaendelea kuwasaidia vijana kupata mitaji itakayowawezesha kuanzisha biashara zao waweze kuwasaidia wengine wasio na ajira na pia kushughulikia changamoto zinazowakabili zikiwamo kutokuaminiwa na taasisi za fedha na kukosa mitaji," anasema Mavunde.





# Tatizo la umeme Dodoma lapatiwa dawa

**Na Peter Mkwavila,**
DODOMA

SHIRIKA la Umeme Tanzania (TANESCO), limesema upatikanaji wa umeme mkoani hapa utaimarika baada ya kukamilika ujenzi wa kituo cha kupozea kilichopo Zuzu, baadaye mwezi huu.

Akikagua ujenzi wa kituo hicho jana, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Shirika hilo, Mhandisi Alexarder Kyaruzi, alisema hatua hiyo itakuwa hivyo baada ya kukamilika na kuzalisha megawati 250.

Alisema hivi sasa kituo kinazalisha megawati 48 ambazo haziwezi kutosheleza kutokana na ongezeko kubwa la watumiaji wa umeme kwa wakazi wa mkoa huo. Mwenyekiti huyo alisema baada ya kukamilika kwa ujenzi huo, kituo hicho kitakuwa na megawati 300, hivyo kutosheleza mahitaji.

Mhandisi Kyaruzi alisema matarajio ya kukamilika kwa ujenzi wa kituo hicho ni Septemba 15, mwaka huu, na ifikapo Septemba 30 wataanza kufanya majaribio ya uzalishaji.

"Hali hii itaongeza upatikanaji wa umeme wa uhakika kwa mkoa wote. Kituo hiki kikikamilika kabisa kitakuwa na umeme mwingi na wenye uhakika, lakini kwa hivi sasa uzalishaji wake ni megawati 48. Kitakapokuwa kimekamilika uzalishaji wake huo utaongezeke na kufikia megawati 250. Huu ni umeme mkubwa na utajitosheleza kwa matumizi ya wakazi wa Dodoma," alisema.

Naye Mratibu wa Mradi wa Ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme kuanzia Tanzania, Kenya na Zambia katika kituo hicho, Mhandisi Peter Kigadye, alisema hadi kukamilika kwa kituo hicho kitakuwa na uwezo wa kupokea umeme wa kilowati 400.

Alisema kwa mwaka 2021 pia mradi huo unatarajia kujenga vituo vya umeme kwenye Wilaya ya Kongwa na Mji wa Kiserikali ikiwa ni jitihada za kuongeza uwezo wa usambazaji wa umeme kwenye maeneo hayo.



Baadhi ya wakazi wa eneo la Kinyasi, Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa, Mkoa wa Dodoma wakipata huduma ya maji kijijini hapo jana. Mkoa huo umekuwa na changamoto ya upatikanaji wa maji kutokana na ukame hasa wakati wa kiangazi. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Mavunde aahidi kujenga shule mpya

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MGOMBEA ubunge wa Jimbo la Dodoma Mjini kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM), Anthony Mavunde, amewahakikishia wananchi endapo atachaguliwa, atajenga shule ya msingi mpya mtaa wa Bwawani, Kata ya Ntyuka ili kuondokana na tatizo la watoto kutembea umbali mrefu kufuata elimu.

Mavunde alitoa ahadi hiyo jana katika kampeni zake kwenye kata hiyo jijini hapa.

Alisema watoto wamekuwa wakitembea umbali mrefu hali inayochangia kushindwa kufanya vizuri kwenye masomo yao, hivyo akichaguliwa atahakikisha kero hiyo inatatuliwa.

"Kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita, nilijenga shule maeneo mengine na kuongeza madarasa na miundombinu mbalimbali ya shule. Mkinichagua tena kwa miaka mingine mitano, nitahakikisha tunamaliza tatizo hilo ili watoto wetu wasome kwenye mazingira rafiki," alisema.

Kuhusu barabara ya Dodoma hadi Mvumi Wilaya ya Chamwino, Mavunde alisema imeombewa kujengwa kwa kiwango cha lami na usanifu wa kitaalamu utaanza mwaka huu.

"Barabara hii kwa miaka mingi sana ilishaombewa ujenzi kwa kiwango cha lami. Nimshukuru mzee wetu Waziri Mkuu mstaafu, John Malecela, ana mchango mkubwa kwenye barabara hii kuhakikisha inajengwa kwa kiwango cha lami na kupitika bila shida muda wote," alisema.

"Leo (jana) nasimama hapa katika historia ya barabara hii. Mwaka huu kwa mara ya kwanza mtashuhudia yakianza mazoezi ya kitaalamu kwa kuanzia pale Kilimani kilometa sita za awali zimetengewa Sh. bilioni sita ambapo utaanza ujenzi wa kiwango cha lami," aliongeza.

Mavunde alisema kero ya miaka mingi ya barabara hiyo kutopitika vizuri, itatatuliwa huku akimshukuru Rais John Magufuli kwa kukubali ombi la ujenzi wa barabara hiyo.

"Taratibu zimebaki chache sana ili kuanza upembuzi yakinifu ili barabara hii yenye kilomita 57 ambapo upande wa Kikombo wameanza na huku Kilimani wameanza itakapokamilika itaondoa kero hii," alisema.

Mavunde pia aliahidi kuwa akichaguliwa atahakikisha maji yanasambazwa kwenye eneo hilo kupitia mradi mkubwa wa Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM).

"Suala la umeme mkinichagua kwa kipindi kingine cha miaka mitano nitahakikisha nitakamilisha usambazaji kwenye maeneo yaliyosalia na kutatua mgogoro wa ardhi kanda ya kijani," alisema.

Aliwahimiza wananchi kujitokeza kwa wingi Oktoba 28 kupiga kura na kukipa ushindi chama hicho kwenye ngazi ya urais, ubunge na udiwani.

# Wazazi wakumbushwa wajibu kuhusu watoto

**Na Peter Mkwavila,** CHAMWINO

WAZAZI katika Wilaya ya Chamwino, mkoani Dodoma, wametakiwa kutimiza wajibu wao kwenye malezi ya wanafunzi wa kike badala ya kuwalazimisha kutumia njia za uzazi wa mpango ili kuwakinga dhidi ya ujauzito.

Mganga wa Kituo cha Afya Mpwayungu, Ambaliche Boniface, aliyasema hayo jana katika kikao kazi cha kupanga mikakati kwenye mradi wa kutokomeza ukatili kwa kupunguza mimba na ndoa za utotoni.

Mradi huo unatekelezwa na Shirika lisilo la Kiserikali la Women Wake Up (WOWAP) kwa ufadhili wa The Foundation For Civil Society.

Dk. Boniface alisema baadhi ya wazazi wamekuwa wakifika kituo cha afya kuomba watoto wao watumie uzazi wa mpango kama njia ya kuwakinga na mimba wakiwa shuleni.

"Mzazi anaona ni bora ampe mtoto wake vidonge vya kupanga uzazi au awekewe kipandikizi au kitanzi. Anaona heri mtoto apate maradhi mengine kuliko mimba," alisema Boniface.

Alisema njia hiyo si salama kwa kuwa mtoto anapowekewa njia za kumkinga dhidi ya ujauzito atazidi kufanya ngono zaidi kwa sababu atajihakikishia yuko huru zaidi.

"Wazazi hawatimizi wajibu wao. Hawakai kwenye nafasi zao, anaona ni heri mtoto afuate uzazi wa mpango. Kama ngono afanye tu ili mradi asipate mimba akafukuzwa shule," alisema.

Alisema watoto wanaofikishwa kituoni hapo ni wale wenye umri wa kuanzia miaka 14 na kuendelea, lakini kituo hicho hakitoa huduma ya kuwafunga watoto uzazi au kutoa vidonge vya uzazi wa mpango.

Kwa sasa, alisema wanashauriana na viongozi wa vijiji ili watoe elimu katika shule za msingi na sekondari ili kuondoa dhana hiyo ambayo imekuwa imeshamiri katika maeneo mengi.

"Si vizuri mtoto wa miaka 14 au 16 kuanza kutumia njia za uzazi wa mpango, anaweza kupata athari za kiafya hapo baadaye," alisema.

Naye Mratibu wa Dawati la Mtoto kutoka Idara ya Maendeleo ya Jamii, Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino, Sophia Swai, alisema tatizo hilo linawakabili watumishi wa kada ya afya walioko kwenye vituo vya afya na zahanati.

"Wao wafuate maadili na miiko ya kazi zao, lakini wawashauri na kuwaambia madhara yake," alisema.

Alisema kutokana na zahanati na vituo vya afya vya serikali kutotoa huduma kwa wanafunzi wanaohitaji huduma, lakini wanaweza kupata huduma kwenye baadhi za zahanati na hospitali zinazokiuka maadili.



# DC ataka amani kampeni uchaguzi

**Na Grace Mwakalinga,** MBARALI

MKUU wa Wilaya ya Mbarali, Reuben Mfune, amewaomba viongozi wa dini, vyama vya siasa, wazee na wasimamizi wa uchaguzi kusimamia na kuhubiri amani katika kipindi hiki cha uchaguzi mkuu.

Mfune aliyasema hayo jana wakati akizungumza na viongozi hao kwenye kikao cha pamoja juu ya namna watakavyohakikisha amani inaendelea kutawala kwenye uchaguzi huo.

Alisema viongozi hao wana nafasi kubwa ya kuhakikisha amani inakuwapo kwa kuwa wana kundi kubwa la watu wanaowaongoza kwa kuiweka ajenda hiyo wakati wanapohubiri neno la Mungu.

"Licha ya kuwa tunahamasisha ushiriki wa wananchi kuchagua viongozi wanaowataka kupitia sanduku la kura ifikapo Oktoba 28, mwaka huu, pia lazima tuhamasishe amani kwa watu wetu ili uchaguzi ufanyike vyema kwa kuhakikisha viongozi hawa wanakuwa mstari wa mbele kuwahimiza watu," alisema Mfune.

Aliongeza kuwa sala na maombi ni nyenzo kuu ambayo italisaidia taifa kufanya uchaguzi wa amani kama ilivyofanyika kipindi cha maambukizi ya virusi vya corona.

"Mtakumbuka viongozi wa dini na wa kisiasa kuwa silaha kubwa tuliyoitumia kuishinda corona ilikuwa maombi. Rais wetu alituhamasisha kila mmoja kwa nafasi yake kumwomba Mungu atuepushe na janga hilo," aliongeza Mfune.

Aliwaomba wagombea wa nafasi za udiwani na ubunge kufuata sheria na taratibu zinazotakiwa kwenye kampeni kwa kuhakikisha zinafanyika kistaarabu na kunadi sera na mipango kwa lugha zenye staha na kwamba atakayekwenda kinyume atafikishwa kwenye vyombo vya sheria.

# Kijana adai kutelekezwa na wazazi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

KIJANA Boniface Mwanjela (21), ambaye ni mlemavu na mkazi wa Mtaa wa Kalobe jijini Mbeya, amewalalamikia wazazi wake kwa madai kuwa wamemtelekeza kutokana na ulemavu wake.

Mwanjela ni mlemavu wa miguu, mikono na anashindwa kujieleza vizuri kutokana na ulimi wake kuwa mzito ili kumwelewa inatakiwa umakini mkubwa kumsikiliza.

Akizungumza na Nipashe jana, kijana huyo ambaye ni mwanafunzi wa kidato cha tatu katika Shule ya Sekondari ya Wavulana ya Iyunga jijini hapa, alisema wazazi wake wote wako hai, lakini hakuna anayemjali na anaishi kwa kutegemea misaada ya wasamaria wema.

Alisema alizaliwa katika Mtaa wa Ikuti, Kata ya Iyunga lakini baadaye wazazi wake waliachana akiwa mdogo, hivyo akaenda kuishi na mama yake Iwambi ambako hata hivyo hawakukaa muda mrefu na mama yake akamtelekeza kwa dada yake wa kufikia aliyekuwa anakaa Kalobe na yeye akaenda kukaa Chunya.

Boniface alisema baba yake aliuza nyumba ambayo walikuwa wanaishi, hivyo kwa sasa hana mahali pa kuishi na badala yake anaishi kwenye nyumba za kupanga hasa kipindi ambacho shule zinakuwa zimefungwa.

"Mama mpaka sasa sina mawasiliano naye maana alienda Chunya. Baba huwa anajisifu kwa watu kuwa ananilea, lakini ni uongo kwa sababu hajui hata ninapokaa. Dada ambaye nilikuwa nakaa naye aliachana na mume wake na yeye akaenda kukaa Njombe," alisema Boniface.

Alisema baada ya kuona hana msaada wa wazazi wake, alikuwa anashindwa kusoma kwa uhuru hali iliyomfanya asiwe anafanya vizuri kwenye masomo yake na kwamba alifeli mtihani wa kidato cha pili mwaka juzi hali iliyomfanya akaamua kutaka kujiua kwa kunywa sumu.

Aliwaomba wasamaria wema wamsaidie ajengewe nyumba ili kuepukana na matatizo ya nyumba za kulipia na kwamba atapata matatizo zaidi atakapokuwa amehitimu kidato cha nne.

Baba mzazi wa Boniface, Mzee Lington Mwanjela, alikiri kutokumhudumia mtoto wake huyo kwa muda mrefu kwa maelezo kuwa hakuwapo kwa kuwa alikuwa Dodoma kutafuta maisha na kwamba amerejea Mbeya hivi karibuni.

Alisema ni kweli aliuza nyumba ambayo alikuwa anaishi na mama yake na kwamba alifanya hivyo kutokana na hasira baada ya mke wake huyo kuondoka na kumwacha na kwamba hata yeye anaumia mtoto wake anapoishi kwenye mazingira magumu.

Alisema huwa anatamani kumsaidia kijana wake na kwamba huwa anaumia sana mtoto huyo anapohangaika, lakini kwa sababu ya umaskini ndio maana huwa anashindwa kumuhudumia ipasavyo.



Baadhi ya wanawake wa Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi mkoani Mbeya, wakiwa wamejitwisha kuni kwa ajili ya matumizi ya nishati ya kupikia majumbani kwao jana, licha ya serikali kupiga marufuku ukataji wa miti holela ili kuepusha uharibifu wa mazingira. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Tulia atumia kauli za bunge kuomba kura

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

NAIBU Spika, Dk. Tulia Ackson, ametumia kauli za michango aliyonukuliwa akichangia bungeni katika vikao vya Bunge la 11 kuomba kura kwa wananchi wa Jiji la Mbeya wakati akizindua kampeni zake za kuwania ubunge katika Jimbo la Mbeya Mjini kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Akizungumza kwenye mkutano wa uzinduzi wa kampeni zake jana kwenye Viwanja vya Ruanda Nzovwe jijini hapa, Dk. Tulia alisema ni yeye aliyekuwa akiwasemea wananchi wa Jiji la Mbeya matatizo yao bungeni na kusababisha serikali ichukue hatua.

Alisema akiwa bungeni, aliomba serikali kutatua kero ya maji na umeme kwenye maeneo mbalimbali kwa kuuliza maswali na serikali kujibu. Ili kuwathibitishia wananchi kuwa ni yeye ndiye aliyekuwa akiwasilisha kero zao bungeni, Dk. Tulia alimtaka 'DJ' kuweka sauti yake aliyokuwa akiuliza maswali bungeni ili wananchi wamsikie.

"DJ hebu piga ile sauti niliyokuwa nikiwaombea wananchi wa Mbeya maji na umeme ili mjue nani alikuwa mtetezi wenu bungeni," alisema Dk. Tulia.

Baada ya kutoa maelezo hayo, DJ akaicheza sauti ya Dk. Tulia ambayo alikuwa anawaombea wananchi wa Kata za Uyole, Itezi, Iyunga, Itagano, Itende na Iwambi na kisha akasikika Naibu Waziri wa Maji, Jumaa Aweso, akijibu.

Kwenye majibu yake, Naibu Waziri Aweso alisema: "Nakushukuru Naibu Spika kwa kuwasemea vizuri wananchi wa Jiji la Mbeya. Nakuhakikishia Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Mbeya imeanza kuchukua hatua za muda mrefu na muda mfupi kuhakikisha maeneo yote uliyoyataja yanapata maji."

Sauti ya pili Dk. Tulia alisikika akiomba baadhi ya Kata za Jiji la Mbeya ambazo ziko pembezoni ikiwamo Nsalaga, Iduda, Nsoho na Mwansekwa wananchi waingiziwe umeme kupitia mradi wa umeme vijijini (Rea) ambao gharama yake ni Sh. 27,000 pekee.

Aidha, kwenye sauti hiyo alisikika Waziri wa Nishati, Dk. Medard Kalemani, alisikika akisema kuwa "Ni kweli baadhi ya maeneo ambayo Naibu Spika umeyataja niliyatembelea hivi karibuni na niliwaahidi wananchi kuwa wataunganishiwa umeme wa Rea."

Dk. Tulia ambaye ndiye mpinzani mkuu wa aliyekuwa Mbunge wa Jimbo hilo, Joseph Mbilinyi 'Sugu' alisema kabla hajawa mbunge alishiriki shughuli za maendeleo katika jiji hilo ikiwamo kuboresha huduma za afya na elimu.

Aliwaomba wananchi kumchagua kuwa mbunge wa jimbo hilo, wawachaguwe madiwani wa kata zote 36 za Jiji la Mbeya wanaotokana na CCM na wamchaguwe Rais John Magufuli ili waendeleze miradi iliyoanzishwa na mingine.

Awali, akizindua kampeni hizo, Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Mbeya, Mchungaji Jacob Mwakasole, alisema baada ya kubaini kuwa serikali ina kasi kubwa kwenye utekelezaji wa ilani ya chama hicho, wameamua kuiongezea ukubwa ilani ya sasa na kuifanya kuwa kubwa zaidi.

Alisema ilani hiyo imesheheni mambo mbalimbali ya maendeleo na inakwenda mpaka mwaka 2030 na hivyo akawataka wananchi kuwachagua wagombea wa CCM.

"Hii Ilani yetu ya sasa ni kubwa kiasi kwamba ukimpa mtoto mdogo akaibeba anaweza akaanguka nayo, sasa nawaombeni wananchi wa Mbeya chaguweni maendeleo," alisema Mwakasole.





# Mwalimu kortini kwa tuhuma za kumtorosha, kubaka mwanafunzi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MWALIMU wa Shule ya Tumbatu Mkoa wa Kaskazini Unguja, Hamad Mdungi (36), amefikishwa katika Mahakama ya Mkokotoni akikabiliwa na mashtaka matatu ikiwamo kumtorosha mwanafunzi wa miaka 14 akiwa chini ya uangalizi wa wazazi wake na kumbaka.

Ilidaiwa jana mahakamani hapo kuwa mtuhumiwa huyo alimtorosha msichana huyo ambaye bado ni mwanafunzi na yupo katika uangalizi wa wazazi wake. Mwendesha Mashtaka kutoka Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP), Ali Juma, mbele ya Hakimu Faraja Shomari alidai kuwa mtuhumiwa alitenda kosa hilo Agosti 17, mwaka huu, Tumbatu Uvuvini, Mkoa wa Kaskazini Unguja. Hakimu Faraja baada ya kusikiliza upande wa mashtaka, aliahirisha kesi hadi Septemba 21, mwaka huu, na kutoa nafasi zaidi kwa upande wa mashahidi kufika mahakamani ili kutoa ushahidi wao.

"Naahirisha kesi hii hadi tarehe 21 mwezi huu ambapo nitawaita mashahidi waje kutoa ushahidi wao ili kesi ianze kusikilizwa kwa wakati," alisema.

Aidha, Hakimu Faraja alikataa dhamana kwa mtuhumiwa huyo na kurudishwa rumande.



Katibu Mtendaji wa Baraza la Habari Tanzania (MCT), Kajubi Mukajanga (kulia), akizungumza na uongozi wa Chuchu Fm, akiwa katika ziara ya kutembelea vyombo vya habari vya Zanzibar jana. Wengine ni Mwenyekiti wa Kamati ya Maadili ya Baraza hilo, Jaji mstaafu Juxon Mlay (pili kulia), Mjumbe wa Bodi ya MCT, Eddah Sanga (wa tatu kulia) na Ofisa wa MCT Zanzibar, Shifaa Said. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# SMZ: Mapambano dawa za kulevya hayana kikomo

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar imesema mapambano dhidi ya dawa za kulevya hayana kikomo na kwamba imejipanga kudhibiti maeneo ya uwanja wa ndege na Bandari ya Malindi kwa kuweka vifaa vya kisasa vya kuchunguza mizigo ya abiria.

Hayo yalisemwa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Mohamed Aboud Mohamed, alipofanya ziara katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume.

Alisema kuwapo kwa vifaa vya kisasa vya uchunguzi wa mizigo inayoingizwa nchini, kwa kiasi kikubwa kutasaidia kudhibiti dawa za kulevya zinazoweza kuingizwa na abiria wanaoingia nchini.

Waziri pia aliwataka wafanyakazi katika uwanja huo kuongeza juhudi na uaminifu kuhakikisha hawarubuniwi na kuruhusu bidhaa haramu zikiwamo dawa za kulevya.

"Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imejizatiti kikamilifu kuhakikisha dawa za kulevya haziingizwi nchini na kusababisha athari kubwa kwa jamii," alisema.

Naye Mkurugenzi wa Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, Hairiyangu Mgeni Khamis, alisema mashine za kukagua mizigo zilizowekwa katika uwanja huo, zimeleta mabadiliko makubwa na kudhibiti uingizaji wa dawa za kulevya.

Alisema katika miezi mitatu iliyopita, watu wawili ambao ni raia wa kigeni wamekamatwa kwa tuhuma za kuingiza dawa za kulevya na waligundulika kwa kutumia mashine zilizowekwa katika uwanja huo.

"Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iko katika mapambano dhidi ya dawa za kulevya. Mkazo umewekwa katika njia kuu za uwanja wa ndege pamoja na bandari kuu ya Malindi na bandari zingine ambazo hutumiwa na wananchi kuingia nchini na mizigo yao," alisema.

Pia alisema juhudi za kudhibiti uingizaji wa dawa za kulevya zinafanywa katika bandari zingine ikiwamo ya Mkokotoni Mkoa wa Kaskazini Unguja na bandari zingine zilizoko Pemba.

"Tumepata mafanikio makubwa katika kudhibiti uingizaji wa dawa za kulevya kupitia katika uwanja wa ndege wa Karume kwa kutumia mashine za kisasa za ukaguzi wa mizigo ya abiria," alisema.

## Watakiwa kuacha aibu unyanyasaji

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WANAWAKE Mkoa wa Kaskazini Unguja wametakiwa kuacha aibu na kutoa taarifa za matukio ya vitendo vya udhalilishaji katika vyombo vya sheria ikiwamo Jeshi la Polisi kwa ajili ya hatua zaidi za kisheria.

Hayo yalielezwa na Mkurugenzi wa Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake (TAMWA) Zanzibar, Dk. Mzuri Issa, wakati akizungumza na wanawake wa mkoa huo kuhusu mikakati ya kupambana na vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia huko Mkokotoni.

Alisema baadhi ya wanawake hawako tayari kutoa taarifa za matukio ya udhalilishaji yanayowakabili kwa hofu ya kuogopa kupewa talaka na waume zao.

"Wanawake msikubali kuficha matukio ya udhalilishaji wa kijinsia ikiwamo ubakaji unaofanywa na jamii wakiwamo ndugu wa familia. Msiogope hofu ya talaka kwa kuficha matukio ya ubakaji," alisema.

Naye mwanaharakati na mfuatiliaji wa kesi za udhalilishaji wa kijinsia Mkoa wa Kaskazini Unguja, Khadija Ali Makame, aliitaka jamii kuwa tayari kutoa ushahidi wa matukio ya kesi za udhalilishaji mahakamani ili kuepuka kesi hizo kufutwa.

Alisema ziko kezi za udhalilishaji wa kijinsia zimefutwa mahakamani kwa sababu jamii haiko tayari kutoa ushahidi utakaowatia hatiani wahusika wa vitendo hivyo.

"Hakuna hatia bila ya ushahidi. Zipo kesi za udhalilishaji wa kijinsia ikiwamo ubakaji zimelazimika kufutwa mahakamani kwa sababu wahusika wake wamekataa kutoa ushahidi," alisema.

Mwanasheria kutoka TAMWA, Zaina Salum Abdalla, alisema vitendo vya ukatili wa kijinsia vimekuwa vikiongezeka kwa sababu jamii yenyewe haipo tayari kuvitokomeza kwa kutoa taarifa katika vyombo vya sheria.

"Njia pekee ya kuvitokomeza vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia ni jamii yenyewe iwe tayari kutoa taarifa mbele ya vyombo vya sheria kwa hatua nyingine za uamuzi," alisema.

Khadija Abdalla, Mratibu wa Wanawake Shehia ya Matetema, alilitaka Jeshi la Polisi kukamilisha upelelezi kwa wakati na kesi kuzipeleka kwa Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) kuanza kusikilizwa.

## MATANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

### VIWANJA/MASHAMBA

**KIWANJA KINAUZWA,** Kiwanja cha Biashara kinauzwa Regent Estate Dsm mita za mraba 1300. Piga; 0693 689996, 0757 129546.


***NIPASHE NI JIBU LAKO***

**NJOO UTANGAZE NASI**

**KWA BEI NAFUU SANA**

**Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0782253676**


### KUPOTEA KWA CHETI



115895602

**ANTHONY R. LUKOO** amepotelewa na Cheti cha elimu ya kidato cha nne alichosomea katika shule ya **EDUCARE SECONDARY,** Alichomaliza mwaka 2013.Na chenye namba ya mtihani: **S. 1200-0071**

Kwa yeyote atakae kiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi,Taarifa ya polisi; **MOR/MOR/RB/654924/2020.**

### KUUNGULIWA NA KADI YA GARI

**Onesmo Semeo Kaiza** anatangaza kuunguliwa na kadi ya gari aina ya Fuso yenye namba za usajili **T 810 BJG.** Kadi hiyo iliungua kwenye kiwanda cha kahawa wilayani Karagwe. Taarifa imefunguliwa kituo cha polisi Bukoba na kupewa RB namba **KAG/BUK/RB/565978/2020.**

115894602

### KUUNGULIWA NA KADI YA GARI

**Onesmo Semeo Kaiza** anatangaza kuunguliwa na kadi ya gari aina ya Fuso yenye namba za usajili **T 263 AYB** kwenye kiwanda cha kahawa wilayani Karagwe. Taarifa imefunguliwa kituo cha polisi Bukoba na kupewa RB namba **KAG/BUK/RB/565988/2020.**

115894602

### KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**JOHN ERASTO MAPIMA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba ya usajili **T 252 CRA** aina ya **TOYOTA ALTEZZA.** Engine **No. 3SEAA1227D** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Taarifa Polisi: **TAN/RB/656110/2020**

115895102

**JAMHURI YA MUUGANO WA TANZANIA**

**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA –MWANZA**

**SHAURI NA 169 LA 2020**

**SAFIA ALLY KOPESHA....................................MDAI**

**DHIDI YA**

1. **LEOPORD KARUGIRA**
2. **MAGDALENA ZABRONI...........................WADAIWA**

**WITO WA KUITWA MAHAKAMANI**

**KWA: LEOPORD KARUGIRA NA MAGDALENA ZABRON**

Mnafahamishwa kwamba mleta maombi hapo juu amefungua shauri/ ombi dhidi yenu katika baraza la ardhi na nyumba mkoa wa mwanza, ombi hili limepangwa kutajwa tarehe 15/09/2019 katika chumba cha baraza ,barabara ya posta jengo liko mkabala na mahakama kuu ya biashara, Tanzania.
Kwa hiyo mnatakiwa kuhudhuria katika baraza siku hiyo nyie mwenyewe, wakili wenu au mtu mwingine anayeruhusiwa kisheria kujibu ombi hilo.
KAA:Mkijua kwamba kushindwa kufika baraza litasikiliza ombi hilo na kutoa uamuzi bila ninyi kuwepo.

**Imetolewa nami kwa Amri na chapa ya Baraza leo tarehe 04/09/2020**

**.......................................**
**MAYETE S.M**
**MWENYEKITI BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA MWANZA**

115895202

### KUPOTEA KWA CHETI



115894502

**DAVIES JOHANES MWAKIPA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha sita chenye index namba **S.3861-0517** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **ANDERLEK RIDGES SEKONDARI** Februari, 2013. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/URA/RB/656173/2020.**

### TANGAZO LA KUPOTEA OFFA YA KIWANJA

**EMMANUEL MIHAMBO** MKAZI WA NDALA MANISPAA YA **SHINYANGA.** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA **OFFA YA KIWANJA NAMBA 81 KITALU "HH" (LD)** KILICHOPO NDALA MANISPAA YA SHINYANGA.

KWA YEYOTE ATAKAE IONA ATOE TAARIFA KWENYE KITUO CHA POLISI KILICHOPO KARIBU, AU AWASILIANE NA EMMANUEL MIHAMBO KWA SIMU NAMBA **0785533412/ 0755297836. RB NAMBA SHY/RB/2020, CONTROL NAMBA 9910818523376.**

115895402

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI FORM II**


**(S.M.M 1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI YA 2)**

**Katika Mahakama ya Mwanzo YA NYALIKUNGU MASWA**

**Usimamizi wa Mirathi Na. 18/2020**

**Ombi la TATU KIDAHA kuteuliwa Msimamizi wa Mirathi ya Marehemu MICHAEL JOHN LINO ANAYEISHI MASWA BIAFRA.**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na Mirathi ya Marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 02/10/2020 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa Mirathi hiyo. Tarehe 9/9/2020.



115895302

THE INTERNATIONAL INSTITUTE OF IOGT-NTO MOVEMENT.

### RIPOTI FUPI YA MAPATO NA MATUMIZI JANUARI - JUNI 2020

| | |
|---|---|
| Salio kutoka mwaka wa fedha 2019 | 14,993,164 |
| KIASI KILICHOPOKELEWA KUTOKA WAFADHILI (TZS) | |
| Jumla Kuu | 644,176,164 |
| MATUMIZI (TZS) | |
| Wafanyakazi | 202,219,119 |
| Matumizi ya ofisi na utawala | 112,767,512 |
| Ujengaji uwezo wa wadau na washirika | 14,414,467 |
| Jumla | 329,401,098 |
| Salio kuu TZS | 329,768,230 |

**JAMHURI YA MUUNGANGO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455.
Fax: +255 26 2323233.
Barua Pepe: ps@mow.go.TZ.
Tovuti: www.mwtc.go.TZ.

Mtaa wa Moshi
S.L.P 2888,
40470DODOMA
09/09/2020

### TANGAZO

Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya **JUMAMOSI tarehe 12-09-2020** Kampuni ya **OTTO MARK INVESTMENT LIMITED** itasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **DAR ES SALAAM kuelekea KAHAMA kupitia VIGWAZA.**

1. Gari hilo lenye namba za usajili zenye vipimo vyake:
   **T 548 CKZ / T 386 CHR**

   **VIPIMO: UREFU 22 UPANA: 4.73 KIMO: 5.2**

2. Gari hizo zinatoka **DAR ES SALAAM** kuelekea **KAHAMA** kupitia **VIGWAZA.**

   Gari itasafiri muda wa mchana tu ***(kuanzia saa 12:30 asubuhi mpaka saa 12:00 jioni).***

*Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.*

115894702

### PASSPORT IMEPOTEA



115895002

**ASHRAF SHAFII MRAMBAS** anatangaza kupotelewa na Hati ya Kusafiria (Passport) yenye namba **TAE 296359** iliyotolewa na Idara ya Uhamiaji Dar es salaam mwaka 2020. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilicho karibu. Taarifa ya polisi: **TAN/TAN/RB/455472/2020.**

### KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**TANZURI SAID MSUYA** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI AINA YA COROLLA SPACIO YENYE NAMBA ZA USAJILI **T 898 DKV.** KWA YOYOTE ATAKAYE IONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI.

TAARIFA YA POLISI: **DAR/KIJ/RB/642510/2020.**

115895702

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI FORM 11**

**(S.M.M.1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)**


**Katika mahakama ya Mwanzo DODOMA MJINI**

**Usimamizi wa Mirathi 114**

**Ombi la HIDAYA HAMISI NGOI kuteuliwa Msimamizi wa Mirathi Marehemu OMARI MOHAMED MWINDUNDU**

**KWA YEYOTE ANAYEHUSIKA TANZANIA BARA**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na Mirathi ya marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 25/09/2020 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa Mirathi hiyo.
Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa Tarehe 09/09/2020.



115895902


***Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa***

***Tupigie 0782253676***



**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**



TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI KITAIFA

# Prof. Lipumba kuwachunguza watuhumiwa 'wasiojulikana'

**Na Boniface Gideon, KIBITI**

MGOMBEA urais kwa tiketi ya CUF, Prof. Ibrahim Lipumba, amesema iwapo Watanzania watampa ridhaa ya kuwa Rais atahakikisha anakomesha na kufanya uchunguzi wa kina juu ya matukio ya uvunjifu wa amani na kupotea kwa watu yanayodaiwa kufanywa na 'wasiojulikana'.

Alitoa kauli hiyo wakati akizungumza na wakazi wa Jimbo la Kibiti mkoani Pwani wakati wa kampeni za kuomba kura jana na kuwanadi wagombea ubunge na udiwani katika Jimbo la Kibiti.

Prof. Lipumba alisema miaka ya hivi karibuni kumekuwapo na matukio ya kupotea kwa watu, lakini hakuna taarifa za kueleweka zinazotoka kwa umma, na kwamba chama hicho kikipata ridhaa ya Watanzania atahakikisha haki za binadamu zinaheshimiwa, ikiwamo wafanya uchunguzi wa kubaini watu hao kwa ajili ya kuchukuliwa hatua zaidi za kisheria.

Prof. Lipumba alisema vitendo vya kihalifu vimekuwa vikishamiri na watu kupotelea kusikojulikana na kutolea mfano watu waliopotea eneo hilo la Kibiti, akiwamo mwandishi wa habari wa kujitegemea wa gazeti la Mwananchi, Azory Gwanda, pamoja na diwani wao wa viti maalumu aliyepotea mwaka 2018 na kuacha mtoto mchanga.

Alisema iwapo Watanzania wataondoa uwoga, itasaidia kujenga nchi inayoheshimu haki za binadamu, ili kukomesha vitendo vya utekaji wa watu na kupotea kusikojulikana kwa kuhakikisha utawala bora unapatikana.

"Watanzania tuchague watu waadilifu wenye mapenzi na binadamu wenzao, tupambane na ugaidi na siyo kuvunja haki za binadamu, watu wengi wamepotea bila kujulikana waliko," alisema na kuongeza:

"Baadhi ya Watanzania wengine wamepata athari ya kupotelewa na ndugu zao, hili si sahihi tunapaswa kuondoa uwoga ndani yetu ili kukomesha hali hii."

"Woga ni adui wa haki hata ndani ya chama chetu, huku Kibiti amewahi kupotezwa mmoja wa kiongozi wetu, tulikwenda mpaka kituo cha sheria na haki za binadamu, lakini hawajawahi kutupa mrejesho juu ya taarifa tulizopeleka dhidi ya kupotea kwa kiongozi huyo," alisema..

Prof. Lipumba alieleza kutofurahishwa na tabia ya baadhi ya viongozi wa serikali kurithishana madaraka kwa watoto wao wakisahau kuwa Watanzania pekee ndio wenye nafasi ya kuchagua kiongozi anayeweza kuwaletea maendeleo kwa maslahi yao.

Alisema tabia ya kurithishana madaraka haina tija kwa Watanzania, hivyo kitendo cha kupeana madaraka wenyewe kwa wenyewe kinawanyima nafasi watu wenye uwezo na nia njema ya kuwatumikia Watanzania ipasavyo. Kiongozi wa kampeni za mgombea huyo, Miraji Mtibwiliko, alisema hali ngumu ya maisha inayowakabili Watanzania wengi nchini inatokana na kuwapa uongozi watu wasiokuwa na uwezo wa kuwatumikia Watanzania.



Nguzo ya simu ikiwa imeanguka kando ya barabara katika eneo la Kigogo Luhanga, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

## Waomba kufidiwa kupisha barabara

**Na Gideon Mwakanosya, SONGEA**

WAKAZI 26 wa Makambi katika Halmashauri ya Manispaa ya Songea mkoani Ruvuma, wameiomba serikali kuwasaidia kulipwa Sh. milioni 46 ambazo ni fidia baada ya kupisha ujenzi wa barabara ya Angoni-Matogoro.

Akizungumza kwa niaba ya wenzake jana, Wilon Kapinga, alidai kuwa tangu mwaka 1986, hawajalipwa fidia licha ya mashamba na nyumba zao kubomolewa kupisha mradi huo.

Alibainisha kuwa kati ya wakazi hao 46, wakazi 18 wanadai fidia za nyuma na wengine wanadai fidia za mimea iliyokuwa kwenye mashamba yao.

Mwakilishi huyo wa wakazi hao, alisema kuwa walilazimika kwenda kumwona Mkuu wa Mkoa Ruvuma, Christina Mndeme, ambaye alipokea malalamiko yao na kuwaelekeza kwamba malalamiko yao wayapeleke kwa Mkuu wa Wilaya ya Songea Mjini, Pololeti Mgema ambaye naye aliwaelekeza waende kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Songea, Tina Sekambo, aliyeahidi kufanyia kazi suala hilo.

Mkurugenzi huyo alipotafutwa na Nipashe jana kuzungumzia suala hilo, alikiri kupokea malalamiko yao na kubainisha kuwa tayari maandalizi ya kuwalipa yalishaanza kufanywa.

Alisema fedha hizo zitalipwa kwa awamu, akibainisha kuwa awamu ya kwanza Halmashauri ya Manispaa ya Songea inatarajia kuwalipa wananchi tisa Sh. milioni 10 na wengine watalipwa kwa awamu nyingine. Mkurugenzi huyo alibainisha kuwa baadhi ya waathirika wa mradi huo walishafariki dunia, hivyo fidia italipwa kwa wasimamizi wa mirathi yao na siyo vinginevyo.

# Mzindakaya aibukia kampeni za Magufuli

**Na Thobias Mwanakatwe,**

**DODOMA**

MWANASIASA mkongwe nchini, Chrisant Mzindakaya, ameibuka na kusema Watanzania wana kila sababu ya kumchagua tena Dk. John Magufuli kuendelea kuwa rais wao kutokana na jinsi alivyowabana wezi wa rasilimali za nchi.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa kampeni za mgombea ubunge wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) katika Jimbo ya Vwawa wilayani Mbozi jana, alisema kuwa baadhi ya wezi hao waliodhibitiwa na Dk. Magufuli walikuwa ni Watanzania wakishirikiana na wenzao wa mataifa ya nje.

"Kuna rafiki yangu juzi ambaye mwekezaji mwenzangu wa huko nje (mzungu)... aliniuliza 'eti mlimpata wapi Dk. Magufuli?' Mimi nilimjibu kwa kifupi tu kuwa 'ni mpango wa Mungu'. Wanauliza hivyo kwa sababu Rais Magufuli amewadhibiti," alisema.

Kuhusu wapinzani kupinga kila kitu, Mzindakaya alisema wanafanya porojo za kihuni kwa kuwa wengi wao wanaujua ukweli wa namna taifa lilivyopita kwenye michakato ya maendeleo hadi kufikia kuingia uchumi wa kati.

Aliwataka Watanzania kote nchini kumwamini na kumchagua tena Dk. Magufuli kwa kuwa kazi aliyoifanya kwa kipindi cha miaka mitano ya uongozi wake imeifanya Tanzania kuheshimika duniani kote.

Alisema serikali ya awamu ya tano imefanikiwa kwa kiasi kikubwa kuandaa, kutekeleza na kusimamia mipango ya kujiletea maendeleo kwa kutumia kikamilifu rasilimali za ndani.

"Zamani ukiwa bungeni na kuuliza swali kuhusu mradi fulani wa maendeleo, utasikia waziri ananyanyuka na kukujibu bado tunazungumza na wahisani, lakini leo bungeni hakuna majibu ya tunangoja wafadhili... Rais Magufuli kayafuta kwa kuwa fedha za ndani zipo na zinatekeleza miradi kwa usawa," alisema.

Aliongeza kuwa fedha zote zinazokusanywa na serikali kama kodi, zimekuwa zikitumika vizuri kwa kupelekwa kwenye shughuli za miradi ya maendeleo kama vile miundombinu ya barabara, elimu na sekta ya afya.

Mzindakaya alisema hali hiyo imechangia kwa kiasi kikubwa utoaji wa huduma kwa jamii kuimarika na kufanya Tanzania kuwa miongoni mwa mataifa vinara wa utoaji huduma Afrika.

Pia, aliwaomba wapigakura wa Vwawa kumpigia kura mgombea ubunge wa jimbo hilo ambaye ni Waziri wa Kilimo, Japhet Hasunga.

Katika mkutano huo, Hasunga alisema kuwa pamoja na kazi kubwa aliyofanya katika sekta za elimu, maji, miundombinu, kilimo na afya, miaka mitano mingine akichaguliwa kuwakilisha jimbo hilo, atamalizia baadhi ya miradi ambayo iko mwishoni na kuboresha zaidi sekta ya elimu.

Alisema Wilaya ya Mbozi ina upungufu wa shule za kidato cha tano na sita, hivyo ndani ya miaka mitano atahakikisha anajenga na kukamilisha shule nne za kidato cha tano na sita ili zifike tano ndani ya jimbo la Vwawa ambalo kwa sasa linayo moja tu ya Vwawa ambayo ni ya wasichana.


## KUMBUKUMBU



215896202

**Familia ya Marehemu Dk. FIRMINA JOSEPH MBERESERO**
**Tarehe ya kuzaliwa: Desemba 13, 1950**
**Tarehe ya kifo: Septemba 11, 2015**

*"Katika uhai wako tulikupenda sana; katika kifo bado tunakupenda. Bado una nafasi katika mioyo yetu ambayo hakuna atakayeweza kuiziba". Mama, ni miaka mitano sasa tangu ulipopumzika na bado tunakumbuka wewe zaidi. Unakumbukwa zaidi na mume wako, watoto wako wa kiume na kike, wajukuu, ndugu na jamaa zako.*

*Katika kumbukizi ya siku hii, kutakuwa na ibada itakayofanyika Septemba 19, 2020 mahali alikozikwa katika shamba la Mtakuja Mangara kuanzia 5:00 asubuhi.*



# MADRID KUMLIPA BALE AONDOKE

**MADRID, Hispania**

REAL Madrid inajiandaa kumlipa Gareth Bale, ili aondoke katika kipindi hiki cha majira ya joto, kwa mujibu wa gazeti la The Telegraph.

Bale amejikuta hayupo kwenye mipango ya Madrid na mara kwa mara amekuwa akihusishwa kuondoka klabuni hapo, licha ya kuwa na mkataba hadi mwaka 2022.


Nyota huyo wa kimataifa wa Wales ambaye analipwa mshahara mkubwa, amekuwa na wakati mgumu kwa mabingwa hao wa LaLiga, lakini sasa wanajiandaa kumlipa ili kuona Bale aondoke.

Kwa mujibu wa ripoti, Real Madrid italipa nusu ya mshahara wa Bale, katika klabu yoyote atakayokwenda, ili kumshawishi aondoke.

Bale amekuwa akihusishwa na mpango wa kurudi kwenye Ligi Kuu England, huku klabu yake ya zamani, Tottenham imeripotiwa kumwania.

Na sasa ni wazi Bale ataondoka Madrid baada ya kukaa na klabu hiyo kwa miaka saba.

## Tonali: Ndoto yangu imetimia



**MILAN, Italia**

SANDRO Tonali ameelezea uhamisho wake wa kwenda kwa miamba wa Ligi Kuu Italia, Serie A, Milan kama ndoto iliyotimia baada ya kuondoka kule Brescia ambayo imeshuka daraja.

Milan ilitangaza kumsajili kinda huyo wa Italia ambaye anatajwa kuwa nyota mkubwa siku za usoni, kwa mkopo huku kukiwa na kipengele cha kumnunua kwa euro milioni 35.

Tonali ni shabiki mkubwa wa Milan tangu akiwa mtoto na sasa akiwa na umri wa miaka 20, kiungo huyo amekamilisha uhamisho wake Jumatano.

"Nina hisia kali na za aina yake. Nina furaha kubwa sana," alisema Tonali akiiambia Sky Sport Italia.

"Kucheza nikiwa na jezi ya Milan ilikuwa ni ndoto yangu kubwa, na sasa nimeshinda ndoto hiyo."

Tonali, ambaye amekuwa akilinganishwa staili yake ya uchezaji na gwiji wa Italia, Andrea Pirlo, alikuwa akihusishwa na mpango wa kuhamia kwa wapinzani wao, Inter Milan.

## Martinez atajwa kutoondoka Inter

**MILAN, Italia**

LAUTARO Martinez hataondoka Inter Milan wakati kukiwa na ripoti za kuwaniwa na Barcelona, Makamu wa Rais wa klabu hiyo, Javier Zanetti, amesema.

Martinez amekuwa akihusishwa sana na uhamisho wa kwenda kwa miamba wa Ligi Kuu Hispania, LaLiga, Barca.

Raia huyo wa Argentina alifunga mabao 21 katika mashindano yote, wakati Inter ikimaliza nafasi ya pili kwenye Serie A na ilifika fainali ya Ligi ya Europa msimu uliopita.

Na raia mwenzake wa Argentina, Zanetti ameondoa uwezekano wa Martinez kuondoka wakati huu wa kuelekea msimu wa 2020-21.

"Lautaro haondoki Inter," amesema Zanetti akiiambia Fox Sports. "Sio tu kwa Barcelona ambao wanamtaka yeye, lakini Lautaro anajua kwamba tayari yupo kwenye klabu kubwa.

"Anaonekana kuwa na furaha na maisha ya nchini Italia, kitu ambacho sio rahisi, nafikiri yupo kwenye njia sahihi.

"Kwa sasa hataondoka. Yeye ni wa kwetu kwa sasa na kwa baadaye. Na kuna heshima kati yetu na ataendelea kuwa wa kwetu tu."

Inter inayonolewa na Antonio Conte itafungua pazia la msimu mpya wa Ligi Kuu Italia, Serie A, nyumbani ikiivaa Fiorentina, Septemba 26, mwaka huu.

HABARI MICHEZO

# NEVILLE

## ATAKA UNITED IMPE SAPOTI SOLSKJAER



**MANCHESTER, England**

GARY Neville ameishauri Manchester United kumuunga mkono Ole Gunnar Solskjaer, katika soko la usajili kama wanataka kutinga kwenye nafasi mbili za juu, katika Ligi Kuu England.

Baada ya kupambana na kumaliza nafasi ya tatu kwenye msimamo wa Ligi Kuu ya England, msimu wa 2019/20, United imemwongeza kiungo Donny van de Beek pekee, kutoka Ajax kwenye kikosi chao.


Nyota wa Borussia Dortmund, Jadon Sancho amekuwa akihusishwa sana na uhamisho wa kwenda Old Trafford, lakini miamba hao wa Ligi Kuu bado hawajakamilisha uhamisho wa fowadi huyo.

Nahodha wa zamani wa United, Neville amesema Solskjaer anahitaji kuungwa mkono kama United ambayo ilimaliza msimu uliopita, ikipitwa pointi 33 na mabingwa Liverpool kama watahitaji kuimarika zaidi.

"Taji na kumaliza kwenye nafasi mbili za juu ndio hatua inayotakiwa kufuatwa. Nafikiri mwaka huu utakuwa mgumu sana, hivyo wanatakiwa kujipanga," amesema.

"Anahitaji wachezaji zaidi na sapoti ya bodi kufanya hivyo. Kama United haitasajili wachezaji, hawatatakiwa kumlaumu kocha kwa kushindwa kutinga kwenye nafasi mbili za juu."

United itaanza kampeni ya Ligi Kuu msimu huu, ikiwa nyumbani kwa kucheza na Crystal Palace, Septemba 19, mwaka huu.



## HAKIMI: CONTE AMENILETA INTER

**MILAN, Italia**

ACHRAF Hakimi amesema "morali ya aina yake" ya Antonio Conte ndio ilikuwa moja ya sababu iliyomhamasisha yeye kujiunga na Inter.

Nyota huyo mwenye umri wa miaka 21, alijiunga na miamba hao wa Serie A Julai, kwa ada iliyoripotiwa kuwa ni euro milioni 40 kutoka kwa mabingwa wa Ligi Kuu Hispania, Real Madrid, na amesaini mkataba wa miaka mitano.

Raia huyo wa Hispania mzaliwa wa Morocco, alitumia misimu miwili akicheza kwa mkopo kule Bundesliga katika klabu ya Borussia Dortmund, na alionyesha kiwango cha kuvutia katika nafasi yake ya mlinzi wa kulia.

Pia, alifunga mabao matano na kutoa pasi za mwisho 10, kwenye Bundesliga msimu uliopita ikiwa takwimu bora zaidi kwa mlinzi.

Conte aliiongoza Inter kumaliza nafasi ya pili, kwenye Ligi Kuu Italia na Hakimi, sasa ameonyesha furaha yake kucheza chini ya kocha huyo, mwenye umri wa miaka 51.

"Nilichagua kuichezea Inter kwa sababu nafikiri staili yake ni nzuri zaidi kwangu mimi kucheza na naweza kuisaidia timu hii," alisema katika wa mahojiano yake na tovuti ya Inter.

"Tutajaribu kutafuta mafanikio kadiri tutakavyoweza na naamini kwa uwezo wa kocha, msimu huu tunaweza kutwaa taji la Ligi Kuu Italia, Scudetto."

# Essien apata ulaji Denmark



**NORTH ZEALAND, Denmark**

KIUNGO wa zamani wa Chelsea, Michael Essien amejiunga na klabu ya FC Nordsjaelland ya Denmark kama kocha na mchezaji kwa ajili ya msimu wa 2020/21.

Nyota huyo mwenye umri wa miaka 37, amekubali kuwa msaidizi wa Kocha Flemming Pedersen kuelekea msimu mpya huku klabu hiyo iliyomaliza katika nafasi ya nane msimu uliopita, ikijipanga kufanya vizuri zaidi msimu huu.

Kiungo huyo wa zamani wa Timu ya Taifa ya Ghana, alikuwa akitarajia kupata nafasi ya kuwa kocha kamili, baada ya kuitumikia timu ya vijana pamoja na akademi.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na klabu hiyo, Essien ataungana na wafanyakazi wengine wa klabu hiyo kusimamia mazoezi pamoja na kukamilisha mipango ya kukijenga kikosi hicho.

Pia, nyota huyo wa zamani wa Lyon na Real Madrid, atachangia katika kutoa uchambuzi kwa njia ya video, ikiwa ni sehemu ya kutoa mafunzo.

Essien, ambaye alitarajiwa kuanza majukumu yake jana, alitumia akaunti zake za mitandao ya jamii kuelezea namna alivyofurahi kupata nafasi katika klabu hiyo.

"Ninafuraha sana kujiunga na benchi la ufundi la FC Nordsjaelland ambalo litakuwa ni njia ya kunipeleka kupata leseni ya kuwa kocha kamili," alisema Essien.

Kiungo huyo alitua Chelsea kwa ada ya pauni milioni 24.4, na kwa muda wa miaka tisa aliyodumu Stamford Bridge, alishinda taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya, mawili ya Ligi Kuu England, manne ya Kombe la FA na moja la Kombe la Ligi.

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# SUAREZ AKANUSHA KUONDOKA BARCA

Afunguka bado anahitaji kuwatumikia vigogo hao wa Hispania na kusitisha ndoto za kutua Juve...

**BARCELONA, Hispania**

LUIS Suarez amebainisha kwamba, kuna "habari za uongo" kuhusu majaliwa yake huku akihusishwa na kuhamia Juventus.

Kocha mpya wa Barcelona, Ronald Koeman, ameripotiwa kumwambia Suarez anaweza kuondoka klabuni hapo na kwamba hayupo kwenye mipango yake ya baadaye, huku rafiki yake mkubwa, Lionel Messi akiamua kubakia kwa Blaugrana hao, baada ya awali kuomba kuondoka.

Suarez amekuwa akitajwa kuwaniwa na Ajax na Inter Miami ya Marekani, lakini akihusishwa na uhamisho wa kwenda kwa mabingwa wa Serie A, Juventus. Lakini mchezaji huyo raia wa Uruguay, aliposti ujumbe kwenye ukurasa wake wa Instagram huku akiendelea na mazoezi pale Barca.

Aliweka picha ikimwonyesha akicheza na huku pia akiweka emoji na aliandika: "Wakati habari za uongo zinapokuja..."

Suarez anashika nafasi ya tatu kwa wafungaji wa wakati wote wa Barca, akipitwa na Messi na Cesar aliyopo nafasi ya pili.

Hata hivyo, Suarez pamoja na Messi sasa wataendelea kubakia Barca kwa msimu mwingine tena, baada ya uhamisho wa kuondoka klabuni kama walivyotarajia kushindikana.

Nyota huyo wa zamani wa Liverpool ameshinda mataji manne ya LaLiga, manne ya Copas del Rey na moja la Ligi ya Mabingwa Ulaya, tangu alipohamia Katalunya mwaka 2014.

Kwa muda wa miaka sita aliokaa Camp Nou, Suarez amecheza mechi 283 za mashindano mbalimbali na kufunga mabao 198 na kutoa pasi za mwisho 97.

## KWA UFUPI

**BARCA YAMTAKA BELLERIN**
BARCELONA imeanza mawasiliano na Arsenal kwa ajili ya kukamilisha mchakato wa kumsajili beki wa Timu ya Taifa ya Hispania, Hector Bellerin. Nyota huyo pia anatakiwa na mabingwa wa Ligi Kuu Ufaransa, Paris St-Germain ambao tayari wameshafanya mawasiliano na wawakilishi wa mchezaji huyo. ***(Sport - in Spanish)***

**RENNES, CHELSEA ZATETA**
KLABU ya Rennes ya Ufaransa imethibitisha kufanya mazungumzo na Chelsea ambayo inahitaji huduma ya golikipa wa Timu ya Taifa ya Senegal, Edouard Mendy (28). ***(Goal)***

**MADRID KUMLIPA BALE**
REAL Madrid iko tayari kulipa nusu ya mshahara wa Gareth Bale (31), kwa ajili ya kurahisisha mchakato wa mshambuliaji huyo wa Timu ya Taifa ya Wales, kuondoka kwa mabingwa hao wa Hispania. ***(Telegraph - subscription required)***

**ARSENAL YAMFUATA AOUAR**
ARSENAL inajiandaa kuwasilisha ofa mpya ya kumsajili kiungo wa Lyon na Timu ya Taifa ya Ufaransa, Houssem Aouar(22), baada ya ile ya awali ya pauni milioni 31.2 kukataliwa. ***(Fabrizio Romano, via ESPN)***

**MARTNEZ AKARIBIA ARSENAL**
ARSENAL inajipanga kuwasilisha ofa ya tatu ya kumwania golikipa wa Aston Villa na Timu ya Taifa ya Argentina, Emiliano Martinez (28), ambaye dau lake ni pauni milioni 20. ***(Mail)***

**KEAN AITAJA JUVE**
STRAIKA wa Everton na Timu ya Taifa ya Italia, Moise Kean (20), anataka kurejea Juventus ikiwa ni mwaka mmoja baada ya kuondoka kwa vigogo hao wa Serie A na kuelekea kwa klabu hiyo maarufu The Toffees. ***(Calciomercato - in Italian)***

**RICHIE KUREJEA BOURNEMOUTH**
KLABU ya Bournemouth inataka kumrejesha klabuni kwake winga wa Timu ya Taifa ya Scotland, Matt Richie akitokea Newcastle United, lakini inakabiliwa na changamoto ya kufikia maslahi binafsi ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30. ***(Newcastle Chronicle)***

**ARSENAL KUMKOSA LUIZ**
BEKI wa kati wa Arsenal na Timu ya Taifa ya Brazil, David Luiz (33), atakuwa nje katika kipindi cha mwezi wa kwanza wa mwanzo wa msimu, kutokana na kupata matatizo ya shingo. ***(Telegraph - subscription required)***

**KING AITAKA UNITED**
WAKATI Aston Villa inataka kumsajili mshambuliaji wa Bournemouth na Timu ya Taifa ya Norway, Joshua King (28), nyota huyo amesema angependelea kujiunga na Manchester United, baada ya mchakato wa kutua Old Trafford kushindikana katika dirisha dogo la usajili la Januari. ***(The Athletic - subscription required)***

**LACAZETTE: BADO NIPO**
MSHAMBULIAJI wa Arsenal na Timu ya Taifa ya Ufaransa, Alexandre Lacazette (29), anatarajia kuweka wazi majukumu aliyonayo katika timu hiyo, ili kuondoa tetesi kwamba, The Gunners imeridhia kumuuza kwenye kipindi cha majira ya joto. ***(ESPN)***

**SOH ANUKIA ENGLAND**
MABOSI wa Nottingham Forest wanajiandaa kumsajili beki wa Paris St-Germain na Timu ya Taifa ya Vijana ya umri chini ya miaka 21 (U-21), Loic Mbe Soh, ambaye ana umri wa miaka 19. ***(Goal - in French)***

**GARNACHO ATUA UNITED**
MANCHESTER United imemsajili, Alejandro Garnacho kutoka Atletico Madrid. Straika huyo mwenye umri wa miaka 16 anatarajiwa kuwasili England akitokea Hispania wiki hii, lakini atalazimika kukaa karantini kwa siku 14. ***(Manchester Evening News)***

## HABARI MICHEZO

# SIMBA SC YAFUNGUKA HAKUNA MECHI RAHISI

**Na Adam Fungamwango**

LICHA ya kuanza msimu mpya wa ushindi, Meneja wa mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba, Patrick Rweyemamu, amesema hawataidharau timu yoyote ile inayoshiriki ligi hiyo na kueleza msimu huu utakuwa mgumu zaidi.

Akizungumza na gazeti hili jana, Rweyemamu alisema, ligi inatarajiwa kuwa na ushindani kwa sababu kila klabu imejiandaa na imejipanga kufanya vema zaidi ya ilivyokuwa katika msimu uliopita.

"Ligi hii inaonekana itakuwa ngumu sana, kuliko hata ya msimu uliopita kutokana na kila mmoja kupania, hili halijifichi," alisema Rweyemamu.

Alisema, Simba imejiandaa vizuri kuelekea mchezo wake dhidi ya Mtibwa Sugar, utakaochezwa kesho kwenye Uwanja wa Jamhuri, Morogoro, lakini kwao kila mechi ni muhimu.

Meneja huyo alisema licha ya kuwa na kipindi kifupi cha usajili na maandalizi, lakini timu zote zimesajili vizuri na kufanya maandalizi ya msingi na anaamini picha ya bingwa itaanza kuonekana kwenye mechi za mzunguko wa kwanza.

"Inaonekana wazi ligi msimu huu, itakuwa na changamoto kubwa. Watu wamepania licha ya kipindi kifupi cha usajili na maandalizi, lakini unaona timu zimesajili vizuri na hata maandalizi yamekuwa makubwa," alisema meneja huyo.

Rweyemamu ambaye timu yake Jumapili iliyopita ilikutana na wakati mgumu, iliposhinda mabao 2-1 dhidi ya Ihefu FC kwenye Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya, amesema kwa sasa hawataidharau timu yoyote ile kwa sababu lengo lao kuu ni ubingwa.

"Tumesafiri na wachezaji wote 28 tuliowasajili, ili kocha awe na wigo mpana wa kuchagua kikosi. Mtibwa ni timu komavu na ngumu kwenye ligi na tunajua watakuja kuonyesha walichonacho, lakini na sisi tunataka ubingwa. Huwezi kuwa bingwa bila kushinda mechi zako," Rweyemamu alisema.

Wakati Simba itakuwa Morogoro, keshokutwa, watani zao Yanga wenyewe watawakaribisha Mbeya City, kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini.




Mshindi wa bonasi ya Jackpot ya SportPesa, Shafii Hassani, akiwa na mfano wa hundi ya Sh. milioni 20.1 aliyokabidhiwa baada ya kubashiri kwa usahihi mechi 12 kati ya 13, kwenye Jackpot ya mechi za mpira wa miguu wiki iliyopita. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Yanga yawapa jeuri Prisons

**Na Saada Akida**

KOCHA Msaidizi wa Tanzania Prisons, Shaaban Kazumba, amesema pointi moja waliyopata ugenini jijini Dar es Salaam, dhidi ya Yanga ni ishara nzuri ya kuendelea kwenye mafanikio katika Ligi Kuu Bara, ambayo ilianza kufanyika wiki iliyopita.

Kazumba alisema kwao matokeo ya sare ya bao 1-1 ni sawa na ushindi na ana imani watakuwa na mwendelezo mzuri katika mechi yao inayofuata dhidi ya KMC FC.

"Tumetoka sare na Yanga, huu ni ushindi, ila hatuwezi kujiamini na kubweteka kwa alama moja, tumefanyia kazi mapungufu yetu kwa ajili ya mechi yetu ijayo, naamini tutakuwa imara zaidi," alisema Kazumba.

Alieleza wanawaheshimu wapinzani wao na wataingia uwanjani kwa tahadhari kwa sababu lengo lao ni kuondoka na pointi tatu muhimu katika mchezo huo.

"Kikosi chetu kipo vizuri, malengo yetu msimu huu ni kuhakikisha tunapata pointi katika kila mechi, hasa ugenini na hili linawezekana kwa sababu timu yetu ina muunganiko mzuri wa wachezaji," alisema kocha huyo.

Aliongeza walifanya usajili kulingana na mapungufu ya msimu uliopita na wachezaji waliowaongeza ni wachache, ambao tayari wameshazoea mfumo wa timu.

Tanzania Prisons itakutana na wenyeji wao KMC FC, ambao wataingia uwanjani wakiwa na kumbukumbu ya ushindi wa mabao 4-0 walioupata dhidi ya Mbeya City.

## Wanariadha Dar walilia maandalizi

**Na Adam Nyangasa, TUDARCO**

TIMU ya Riadha ya Mkoa wa Dar es Salaam imeutupia lawama uongozi wao kwa kutowapa maandalizi sahihi kuelekea mashindano ya Taifa ya mchezo huo, yanayotarajiwa kufanyika kuanzia kesho jijini hapa.

Wakizungumza na gazeti hili kwenye mazoezi ya timu hiyo jijini jana, mmoja wa wanariadha hao (jina tunalihifadhi), alisema kambi yao imekuwa ikifanya mazoezi katika hali ngumu, jambo ambalo linawakatisha tamaa.

Mwanariadha huyo alisema timu yao haijapata ushirikiano kutoka kwa viongozi, kama zilivyo timu nyingine zinazotarajiwa kushiriki michuano hiyo.

"Mpaka sasa timu ya mkoa haijakaa kambini, licha ya kuwa na siku chache tu kabla ya mashindano hayo ya kitaifa hayajaanza," alisema mwanariadha huyo ambaye anakimbia mbio za mita 400 na mita 200. Mwanariadha mwingine alisema hadi kufikia juzi jioni, hakuna kiongozi yeyote aliyekwenda kuitembelea timu hiyo, ambayo inatakiwa kupeperusha vema bendera ya mkoa kwenye mashindano hayo ya Taifa.

"Hatujaona uongozi wa mkoa, hakuna kiongozi wa michezo ngazi ya mkoa, aliyekuja kutuona, sisi tuko kama yatima, sio kama walivyo wenzetu," alisema mchezaji huyo.

Aliongeza kuwa timu yao inafanya mazoezi bila ya vifaa muhimu na vile vile haina maji. Nyota huyo aliongeza kwa kuwataka wadau wa riadha na michezo nchini kuisaidia timu hiyo, ili itimize malengo yake ya kufanya vizuri katika michuano hiyo.

## Namungo yatamba kuendeleza ubabe

**Na Shufaa Lyimo**

IKIWA bado kwenye uwanja wa nyumbani mkoani Lindi, Kocha Mkuu wa Namungo FC, Hitimana Thierry, amesema wamejipanga kuendeleza ubabe katika mchezo wao unaofuata wa Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Polisi Tanzania, utakaochezwa Septemba 14, mwaka huu.

Hitimana alisema wachezaji wake wako tayari kwa ajili ya mchezo huo na lengo ni kupata pointi tatu zitakazowaweka kwenye nafasi nzuri, katika msimamo wa ligi hiyo.

"Tunaupa umuhimu mkubwa mchezo wetu wa pili, tumejipanga kuendeleza ushindani katika ligi hii, kwa sababu tunatambua Polisi Tanzania ni moja ya timu ngumu ambayo ina wachezaji wazuri," alisema Hitimana.

Kocha huyo aliongeza msimu huu ni mgumu na wenye ushindani tofauti na msimu uliopita, na amewaandaa wachezaji wake kupambana katika kila mechi.

"Tunaendelea na mazoezi kuhakikisha katika mchezo huo tunapambana mpaka pointi tatu zibakie hapa nyumbani," alisema kocha huyo.

Aliongeza kupungua kwa idadi ya timu kwenye ligi hiyo kumeongeza changamoto na amewataka wachezaji wake kuongeza umakini wanapokuwa na mpira.

Namungo ambayo msimu uliopita ilicheza fainali ya mashindano ya Kombe la FA dhidi ya mabingwa Simba, ilianza msimu wa 2020/21 kwa ushindi, baada ya kuifunga Coastal Union ya jijini, Tanga bao 1-0.

Michezo
Ijumaa Septemba 11, 2020
Nipashe



SUAREZ AKANUSHA KUONDOKA BARCA HABARI UK 22

## ZLATKO ABAINI NJIA YA USHINDI

Na Saada Akida

KOCHA Mkuu wa Yanga, Zlatko Krmpotic, amesema tayari amefahamu mbinu itakayoisadia timu yake kupata ushindi katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Mbeya City itakayochezwa keshokutwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini, Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Zlatko, alisema kila mchezaji wa Yanga ana 'kitu cha kipekee' jambo ambalo ameliboresha na ana imani itasaidia kuibuka na pointi tatu katika mchezo huo wa raundi ya pili.

Zlatko alisema kikosi hicho kinaendelea vizuri na wachezaji watakuwa katika kiwango anachokitaka ndani ya muda mfupi ujao.

"Kuna vitu nimeviona kwa wachezaji wangu, hicho kinakipa imani baada ya muda watakuwa tayari kutoa kilicho bora, najua tunatakiwa kupambana wakati huo huo nikiijenga timu imara na ya ushindani," alisema Zlatko.

Kocha huyo alisema bado yuko katika mchakato wa kuijenga timu hiyo ili ipate muunganiko bora baada ya kuhakikisha kila mchezaji amekuwa 'fiti' na tayari kupambana kwa dakika zote za mchezo.

"Kwa sasa wanashindwa kuonyesha ubora wao kwa kuwa bado hawajawa na muunganiko mzuri, namna wachezaji hawa wanavyocheza, wanaonyesha wana kitu katika ubora wao, imani yangu ni kwamba baada ya muda watakuwa tayari kutoa kilicho bora na ndicho tunachokihitaji," kocha huyo alisema.

Alisema baada ya kufanyia kazi mapungufu ya mechi iliyopita, ameona mabadiliko kwenye mazoezi yanayoendelea na anafurahishwa na ushindani unaoonyeshwa kwenye kila programu anayowapa.

"Mwanzo wa sare sio mbaya, nimeona namna ambavyo wachezaji walikuwa wakicheza kwa kuwa ni mchezo wa kwanza huwezi kulaumu, kinachofuata kwa sasa ni kuendelea kujipanga kwa ajili ya mechi zinazofuata, bado ni mapema kusema lolote, tunatatajia kufanya vizuri msimu huu, tunahitaji muda na utulivu," Zlatko aliongeza. Alieleza pia anahitaji kuona nyota wake wanaongeza umakini, hasa kwenye safu ya ushambuliaji ili kutumia vema nafasi zote wanazozitengeneza.

Naye mshauri wa timu hiyo, Senzo Masingisa, amewataka mashabiki na wanachama wa Yanga kuendelea kushikamana ili kuhakikisha klabu yao inapata mafanikio.

Senzo alisema mashabiki wanatakiwa kuisapoti timu yao na kusahau changamoto za msimu uliopita.



Rais wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Wallace Karia (kushoto), akimpongeza Mwenyekiti wa Soka Wilaya ya Kinondoni (KIFA), Salim Mwaking'inda (kulia), baada ya kupokea mipira 50 iliyotolewa na Mjumbe wa Kamati ya Utendaji ya shirikisho hilo, Lameck Nyambaya (katikati). Nyambaya ametoa mipira 250 kwa wilaya zote za jijini Dar es Salaam, jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# VILLA YAJIANDAA KUMUUZA SAMATTA

●●●Ni baada ya klabu hiyo kusajili mastraika wapya akiwa amedumu England kwa muda wa miezi...

**LONDON, England**

NAHODHA wa Timu ya Taifa ya Tanzania (Taifa Stars), Mbwana Samatta ambaye alijiunga na Aston Villa Januari mwaka huu chini ya kocha Dean Smith anatarajiwa kuondoka katika klabu hiyo kabla ya dirisha la usajili kufungwa.

Mshambuliaji huyo alijiunga na Villa akitokea Genk kwa ada ya pauni milioni 8.5, kama mbadala wa Wesley aliyekuwa majeruhi, lakini sasa anaonekana kukosa nafasi baada ya ujio wa straika mpya, Ollie Watkins ambaye ametua kwa dau la pauni milioni 33.

Taarifa kutoka Uturuki zinasema klabu ya Besiktas imeonyesha nia ya kumsajili mshambuliaji huyo wa zamani wa Simba, African Lyon za Tanzania na TP Mazembe ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), ambaye ana umri wa miaka 27.

Watkins ametua rasmi Villa juzi Jumatano akitokea katika klabu ya Ligi Daraja la Kwanza nchini England, Brentford.

Huku Smith akiendelea kusaka straika mwingine, gazeti la Sportsmail linafahamu Samatta ni mmoja kati ya



wachezaji wanaotakiwa kuondoka klabuni hapo kabla ya dirisha la usajili kufungwa ifikapo Oktoba 4, mwaka huu.

Kiungo, Marvelous Nakamba, mabeki Bjorn Engels na Frederic Guilbert na magolikipa, Orjan Nyland na Lovre Kalinic wanatajwa wataendelea kuitumikia klabu hiyo sambamba na mshambuliaji, Scott Hogan, huku Villa ikitajwa kuwasilisha ofa ya kumsajili, Anwar El Ghazi kama Smith atahitaji kuongeza wigo wa washambuliaji.

Hogan alionekana kuwa na msimu mzuri wa mkopo alipokuwa kwa wapinzani wa Villa, kikosi cha Birmingham kwenye mzunguko wa pili wa msimu uliopita.

Samatta, Nakamba, Engels, Kalinic na Guilbert walisajiliwa wakati Jesus Garcia Pitarch akiwa Mkurugenzi wa Michezo wa klabu hiyo, ambaye alitumia kiasi cha pauni milioni 140 kwa ajili ya usajili wa nyota hao na wa kipindi kilichopita cha majira ya joto.

Garcia Pitarch maarufu kwa jina la Suso aliondolewa kwenye nafasi hiyo mwishoni mwa msimu uliopita baada ya klabu kutoridhishwa na mipango ya utendaji wake wa kazi.

Nafasi ya Suso imechukuliwa na Johan Lange, huku Villa pia ikimwajiri skauti wa zamani wa Leicester na Tottenham, Rob Mackenzie kama Mkuu wa Idara ya Usajili.

Katika kujiimarisha, Villa pia ilikuwa na mpango wa kumsajili mshambuliaji wa Bournemouth, Callum Wilson, ambaye amemwaga wino katika klabu ya Newcastle United.

Villa ilipata mashabiki kutoka Tanzania na nchi jirani za Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati baada ya kumsajili Samatta ambaye mwaka jana aliiongoza Taifa Stars kwenye fainali za Kombe la Afrika (AFCON 2019), zilizofanyika nchini Misri.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002 >